## MADENI YA BIL. 981.8/- YAFUTWA KISA NYARAKA UK. 4



**SAMIA** ataja mambo 10 kwa mageuzi uvuvi

UKURASA 3

**DC** akalia kuti kavu kutukana wananchi

UKURASA 4

**NMB** yaweka rekodi mpya ikipata faida ya bil. 775/-

UKURASA 4



**KOCHA WA IVORY COAST ASEMA HAKUNA KULALA**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatano Januari 31, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581572

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Ma-DED njiapanda kusimamia uchaguzi

**KAMATI** ya Bunge yapendekeza awe mtumishi yeyote, yataka... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akielezea kuhusu aina mbalimbali za samaki, wanaopatikana katika Ziwa Victoria baada ya kuzindua boti za kisasa na vizimba vya kufugia samaki jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, wakitumia kamba kuwavusha wananchi wa maeneo ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro, baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji ya mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Zimamoto waingia mitaani kuwaokoa waathirika mafuriko

UKURASA 2

# Mbaroni madai kutapeli padri kwa kujifanya ofisa wa polisi

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA: GUEDE SI MRITHI WA MAYELE UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akiteta jambo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Ma-DED njiapanda kusimamia uchaguzi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, imependekeza sheria mpya ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023 inayotungwa na Bunge, isiweke ulazima kwa wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kusimamia uchaguzi.

Badala yake, imependekeza kuwapo masharti ya mtumishi wa umma mwandamizi au mtu mwingine yoyote mwenye sifa, kuteuliwa kuwa msimamizi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo Bungeni jana, jijini hapa, Dk. Joseph Mhagama ambaye ni mwenyekiti wake, alisema kamati inaona hakuna ulazima wa sheria kuweka sharti kwa wakurugenzi wa majiji, manispaa, miji na halmashauri za wilaya kuwa wasimamizi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi, kwa kuwa uzoefu unaonyesha wako wakurugenzi, kwa sababu mbalimbali wanapoteza sifa za kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa Dk. Mhagama, Mahakama ya Rufani ya Tanzania, kwenye kesi ya madai namba 138/2019 na Mahakama ya Afrika ya Watu na Haki za Binadamu kwenye kesi ya madai, namba 11/2020, ziliamua kuwa wakurugenzi kusimamia uchaguzi hakukiuki masharti ya Katiba wala Mkataba wa Afrika wa Watu na Haki za Binadamu mtawalia.

Hata hivyo, hoja 58 zilizowasilishwa na wadau mbalimbali, wakati wa mchakato wa ukusanyaji maoni; Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilipendekeza jina la muswada huo lisomeke 'Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji.

Aidha, Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Kituo cha Sheria na Msaada wa Haki za Binadamu (LHRC), Twaweza, Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), walitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ipewe jukumu la kusimamia uchaguzi mkuu wa serikali za mitaa.

Aidha, CHADEMA, ilisema kifungu cha 5 cha sheria hiyo hakijaondoa changamoto ya uundwaji wa majimbo ya uchaguzi kwa kutumia kigezo cha uwiano wa idadi ya watu na kwamba bado mamlaka ya mwisho ya kuidhinisha mipaka na mgawanyo wa majimbo ya uchaguzi yameachwa kwa Rais, ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa CCM ambaye anaweza kuwa mgombea wa nafasi ya urais.

Pia katika ibara ya 6, Chama cha ACT Wazalendo, ilipendekeza kifungu hicho kirekebishwe kwa kuwa wakurugenzi wa sasa ni wanasiasa walioshindwa uchaguzi wakateuliwa kwenye nafasi hizo.

**UNYANYASAJI KINGONO**

Katika sheria inayopendekezwa, kamati hiyo imeshauri kuanzisha kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia wakati wa uchaguzi kuwa ni kosa wakati wa uchaguzi kwa kuwa unafifisha jitihada za kitaifa kufikia usawa wa malengo ya uwiano wa 50/50 katika uongozi.

Pamoja na mambo mengine, kamati hiyo imeipongeza serikali kwa kuweka ibara ya 52 inayoweka masharti ya mgombea ubunge kutoteuliwa katika nafasi zaidi ya moja au nafasi nyingine yoyote ya kuchaguliwa hasa udiwani.

Kamati hiyo pia imependekeza kuanzishwa kwa mfumo wa upatikanaji wa wabunge na madiwani wa Viti Maalum, ikisema kukosekana kwa mfumo mahususi wa wazi kwa vyama vya siasa, kuteua wawakilishi wa makundi hayo, kunachochea rushwa.

**SHERIA KUUNGANISHWA**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenista Mhagama, alisema muswada wa sheria inayotungwa, inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

"Kutungwa kwa sheria inayopendekezwa, ambayo itaunganisha masharti yote katika sheria moja, kutasaidia usimamizi na utekelezaji wa masharti hayo, ikizingatiwa kuwa sheria hizo mbili hutekelezwa na mamlaka moja, ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi," alisema.

Alisema muswada huo unakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kutokana na masharti ya sheria hizo kufanana na kutengeneza sheria moja ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Muswada huo, alisema unaweka masharti kuhusu uandikishaji wa wapigakura ikiwamo kuainisha sifa za mtu kuandikishwa au kukosa sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura, sehemu ya kupigia kura na masharti kuhusu Daftari la Awali na Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Waziri huyo pia alisema muswada huo pia unaweka masharti kuhusu uchaguzi wa Rais, ambaye ni mgombea urais kudhaminiwa kwa maandishi na wadhamini walioandikishwa kuwa wapigakura wasiopungua 200 kwa kila mkoa, angalau kwa mikoa 10 Tanzania Bara na miwili Zanzibar.

Kwa mujibu wa muswada huo, wadhamini watatakiwa kumdhamini mgombea mmoja na ambaye atadhamini mgombea zaidi ya mmoja kwa kujua au kutokujua, watatozwa faini ya isiyopungua Sh. 200,000.

Aidha, muswada huo unapendekeza kuwa Tume ya Uchaguzi, kutoa fomu za uteuzi kwa mgombea wa kiti cha Rais aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi na kwa idadi kadri itakavyoelekezwa na tume.

Katika ubunge na udiwani, muswada huo umeainisha sifa za wagombea katika uchaguzi, siku ya uteuzi, uteuzi wa wagombea, utaratibu wa namna ya kuweka dhamana kwa mgombea, masharti ya mgombea kuteuliwa kwa jimbo moja tu, pingamizi na utaratibu wa kufuatwa endapo kuna mgombea mmoja tu halali wa nafasi ya ubunge au endapo hakuna mgombea.

Mhagama pia alisema muswada huo umeainisha makosa ya uchaguzi ambayo kutumia wadhifa kushawishi watu wengine kutoomba kuteuliwa, mwenendo usiofaa wa watendaji wa uchaguzi na maofisa waandikishaji, makosa yanayohusu fomu za uteuzi au karatasi za kura na vitendo vya ushawishi na rushwa.

Makosa mengine ni kutotunza siri katika uchaguzi kwa watu wanaoruhusiwa kuwa katika kituo cha kupigia kura au kuhesabia kura.

Kwa mujibu wa muswada adhabu za makosa hayo ni kuanzia faini ya Sh. 50,000, Sh. 100,000 hadi Sh. 300,000 au kifungo kisichopungua miezi 12 au vyote kwa pamoja.

Pia muswada huo umeongeza kifungu kipya kidogo kinachoweka adhabu ya faini isiyozidi Sh. milioni 20, kwa chama cha siasa kitakachomruhusu mtu asiye raia kushiriki katika mchakato wa chama katika kufanya uamuzi wake.

## Zimamoto waingia mtaani kuokoa waathirika wa mafuriko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro linafanyakazi ya kuokoa maisha ya wananchi wa mitaa ya kata ya Kihonda na Lukobe, baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji ya mvua inayoendelea kunyesha toka usiku wa kuamkia Januari 30.

Kamanda wa Jeshi hilo Mkoa wa Morogoro, Shaaban Malugujo, alisema shughuli za uokoaji zimefanyika kuanzia asubuhi ya Januari 30, baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha adha kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mvua hiyo ilisababisha wananchi kukwama kutoka katika maeneo yao kwenda kwenye shughuli za uzalishaji wakiwamo wanafunzi.

Alisema askari wa jeshi hilo walipofika eneo hilo walilazimika kuwavusha kwa kutumia kamba wananchi wanaotumia barabara ya Mazimbu, Kata ya Kihonda na Lukobe, wengine waliwabeba watoto kutokana na barabara kujaa maji.

Malugujo alisema jeshi hilo limewaokoa watu saba waliozingirwa na maji katika Mtaa wa Kihonda kwa Chambo na kuwafikisha maeneo salama.

Kamanda wa Jeshi hilo alitaja maeneo yaliathiriwa kuwa ni Kihonda kwa Chambo, Kihonda kwa Bwana Jela na mitaa ya kata ya Lukobe.

"Kwa kweli niwapongeze askari wetu wamefanya juhudi kubwa za kuwaokoa wananchi ambao makazi yao yamezingirwa na maji hususani eneo la Kihonda kwa Chambo kwa kuvushwa kwa njia ya kamba na wengine kubebwa wakiwamo watoto," alisema Malugujo.

Mmoja wa wakazi wa eneo la Kihonda kwa Chambo ambaye nyumba yake ilizingirwa na maji, Sudi Ramadhani, alisema mvua ilionyesha usiku wa Januari 30 imesababisha maji kuingia ndani na kufanya uharibifu wa vitu mbalimbali na vingine kusombwa kuelekea kusikojulikana na kwamba wao walipata msaada wa kuokolewa kutoka askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Januari 29, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitoa matarajio ya hali mbaya ya hewa kwa angalizo la mvua kubwa katika maeneo machache ya mikoa ya Morogoro, Lindi, Mtwara, Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe na Ruvuma.

Kwa mujibu wa angalizo hilo athari zinazoweza kujitokeza ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji pamoja na kuathirika kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi.

Januari 25, mwaka huu mvua kubwa ya mafuriko ilinyesha Manispaa ya Morogoro na kusababisha vifo huku kaya 157 zenye jumla ya zaidi ya watu 246 ziliokolewa na kupelekwa maeneo salama.

# Samia ataja mambo 10 mageuzi sekta uvuvi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan amebaini mambo 10 yanayoendelea kufanywa na serikali kuinua uchumi unaotokana na sekta ya uvuvi na kuongeza mchango katika Pato la Taifa kutoka asilimia 1.8 hadi 10 ifikapo 2030.

Rais Samia alibainisha hayo jana mkoani hapa katika hotuba yake ya zaidi ya nusu saa wakati wa hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vizimba vya ufugaji wa samaki na boti za kisasa kwa wavuvi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuonesha kutokuridhishwa na pato linalopatikana katika sekta hiyo.

"Pato la asilimia 1.8 kwa rasilimali za mito, maziwa pamoja na bahari tulizonazo katika taifa letu ni kidogo sana, hivyo tumedhamiria kuendelea kuboresha sekta hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunafanya mageuzi na kuongeza mauzo ndani na nje ya nchi," alisema Rais.

Miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kufanywa na serikali pamoja na yanayoendelea kutekelezwa ili sekta hiyo inakuwa na mchango mkubwa katika taifa ni pamoja na kuimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Uvuvi.

Katika kuimarisha wizara hiyo, alisema alimkabidhi waziri mwenye dhamana na kumpa miezi sita ya kufanya mabadiliko katika maeneo mbalimbali ambayo tayari yameanza kuonekana kwa sekta hiyo kuanza kutoa mikopo ya zana kwa wavuvi.

Pia serikali inaendelea na mpango wa kuweka miundo ya wawekezaji kibiashara kutoka ndani na nje ya nchi ili kuisaidia sekta hiyo kuongeza uzalishaji pamoja na mauzo na kuinua uchumi wa taifa na wananchi wanaofanya kazi katika sekta hiyo.

Rais Samia alipokea na kukubali mpango wa wizara hiyo kuweka chombo/wakala atakayesimamia na kuangalia maendeleo ya sekta ya uvuvi na kuwaondolea adha wavuvi pamoja na wafanyabiashara kulazimika kuifikia wizara katika utatuzi wa changamoto pamoja na mipango ya sekta hiyo.

"Katika ombi hili ni lazima kwanza lifanyiwe wasilisho serikali tulipitie na kulifanyia maamuzi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha halileti athari katika ung'atuzi wa madaraka kutoka katika Wizara ya TAMISEMI inayosimamia maofisa uvuvi," alisisitiza Rais Samia.

Pia alisema katika kuhakikisha sekta hiyo inatoa mchango mkubwa kwa jamii, serikali itahakikisha inarasimisha ajira zilizopo ndani ya sekta hiyo wakiwamo vijana na wanawake ambazo hapo awali zilitambulika kama ajira zisizo rasmi kwa muda mrefu.

"Itakuwapo kanzi data kwa ajili ya kuwatambua na kuweka rekodi ya wavuvi wote, wafugaji wa rasilimali maji, wachakataji wa mazao ya samaki pamoja na wafanyabiashara..." alisema.

Pia alisema serikali imeanza na itaendelea kutoa zana za kisasa za uvuvi na ufugaji kwa makundi mbalimbali wakiwamo vijana na wanawake. Mradi wa kugawa boti 160 ulizinduliwa jana kwa nchi nzima na 55 zikitolewa kwa wavuvi wa Kanda ya Ziwa.

Alisema serikali itaendelea kuongeza zana hizo kulingana na matokeo yatakayopatikana kutoka kwa wanufaika hao wa awali wa mradi huo.

Vilevile, ujenzi wa bandari kubwa za uvuvi katika ukanda wa Afrika Mashariki ambazo pia zinaendelea kujengwa Kilwa na Bagamoyo kujenga miundombinu ya usafirishaji ikiwamo barabara, viwanja vya ndege ukiwamo wa Mwanza ambao utakuwa ukisafirisha mazao hayo na maeneo ya kuhifadhia.

Pia alitaja mpango wa ununuzi wa meli za kisasa za uvuvi, ujenzi wa vituo vya kuendeleza ufugaji wa viumbe maji, mashamba darasa ya ufugaji wa uvuvi pamoja kuongeza bajeti katika Wizara ya Uvuvi na Ufugaji itakayoenda sambamba na kutangaza uwekezaji wa sekta hiyo.

"Tutahakikisha umeme unapatikana wakati wote kwani bado tunaendelea kufanya maboresho yatakayosaidia tatizo hilo kwisha kabisa na kuwezesha shughuli za uwekezaji," alisisitiza.

Awali, Waziri wa Uvuvi na Ufugaji, Abdallah Ulega, alisema mkopo wa boti hizo 160 zikiwamo 55 zilizotolewa kwa wavuvi 989 Kanda ya Ziwa na vizimba 222 vya ufugaji samaki vyenye vifaranga, chakula na samaki umetolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) bila riba.

Alisema mkopo huo umetolewa kwa makundi ya wavuvi wadogo wakiwamo vijana na wanawake baada ya kubaini kuwa zaidi ya asilimia 95 ya wavuvi nchini ni wadogo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla alisema uzalishaji wa mazao ya samaki katika Ziwa Victoria umekuwa ukiathiriwa na uvuvi haramu hali ambayo imewalazimu kuweka vikao na wavuvi na kuweka mikakati 11 kwa ajili ya kudhibiti vitendo hivyo.

Alisema ili kukuza sekta hiyo kwa Kanda ya Ziwa, wakuu wote wa mikoa inayozunguka ziwa hilo wameweka mkakati mahususi wa kudhibiti uvuvi haramu utakaosaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya samaki katika ziwa hilo.

Christine Mtenya mmoja wa wanufaika wa mradi huo aliomba serikali kuboresha miundombinu ya ufugaji na uvuvi ikiwa ni pamoja kutoa mbegu bora za samaki wa kisasa ili kupata uvunaji wa haraka utakaowasaidia kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.



Baadhi ya nyumba zilizojengwa kando ya mto eneo la Mabibo zikiwa zimebomoka kutokana na mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mbaroni madai ya kumtapeli padri akijifanya ofisa polisi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu wanane kwa tuhuma, akiwamo mmoja kwa kujifanya ofisa wa polisi na kujaribu kumtapeli padri wa Kanisa Katoliki.

Aidha, jeshi hilo linawashikilia watu wengine watatu kwa tuhuma za utapeli na wengine wanne kwa madai ya kukutwa na fuvu la kichwa cha binadamu, ngozi ya mnyama na pembe za ndovu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Marco Chilya, alisema mkazi wa kijiji cha Litola wilayani Namtumbo, Felician Mgomela (40), akijifanya kuwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wilayani humo, alimtuhumu Padri John Otete wa Parokia ya Ifinga, Madaba, Songea, kuwa anajihusisha na biashara ya nyara za serikali, hivyo kumtaka kukutana naye ili amsaidie.

Aliwataja wengine waliokamatwa kwa madai ya utapeli ni Raymond Maige (35) mkazi wa Mtarawe, Damiani Chiwangu (34) mkazi wa Mjimwema na Frank Kiluka (26) mkazi wa Matomondo wilayani Songea.

Kamanda Chilya alisema Mgomela alikamatwa Januari 17, mwaka huu majira ya saa 4:00 asubuhi katika eneo la Njiapanda ya Chandamali, Kata ya Seedfarm, Manispaa ya Songea, wakitaka kumtapeli Padri Otete.

Alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa Mgomela aliwahi kuwatapeli watu wengine akiwamo mtawa wa kiume, Ponsiano Ndunguru, na wanafunzi wengine wanne wote wa seminari ya Lighano kwa kuwatishia kuwa wanajihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Kamanda Chilya alisema mtu huyo alichukua mali zao zikiwamo simu aina ya Samsung Galaxy Note 10, Techno Pop3, Techno ya Tochi, Infinix Hot 10, Iteli, saa mkononi, Earphone na Sh. 15,000 kisha kutokomea nazo na kwenda kusikojulikana.

Pia alisema Januari 4, mwaka huu, majira ya saa 10:00 jioni katika eneo la Mfaranyaki, Manispaa ya Songea, polisi walimkamata Kiluka anayedaiwa kumtapeli Mariamu Lazaro na kuchukua Sh. milioni sita kwa makubaliano ya kumletea gari aina ya Toyota Brevis kutoka Dar es Salaam.

Alisema baada ya mtuhumiwa kuchukua fedha hizo, alibadili namba ya simu na kutokomea kusikojulikana ndipo Mariamu aliporipoti polisi na hatimaye kukamatwa na kugundua alimtapeli mtumishi wa benki Sh. milioni 35.265 kwa makubaliano ya kumuuzia magunia 400 ya mahindi lakini alitokomea na fedha hizo kusikojulikana.

Kamanda Chilya alisema upelelezi wa kina ulibaini kuwa mtuhumiwa huyo amekuwa akiwatapeli wanawake wafanyabiashara na wajane kwa kuwalaghai kufanya nao biashara mbalimbali kisha kuwachukulia fedha na kutokomea nazo kusikojulikana.

Katika tukio jingine lililotokea Januari 2, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi katika eneo la mgahawa wa Krista Park Manispaa ya Songea, askari kanzu walikamata watuhumiwa Raymond Maige (35) mkazi wa Matarawe, Songea na Damiani Everinus (34) mkazi wa Mjimwema, Songea baada ya kumtapeli Henry Msigwa kwa kujifanya kuwa wao ni maofisa wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) wenye vyeo vya kapteni na kuchukua Sh. 500,000 ili wamsaidie mdogo wa mfanyabiashara huyo kujiunga na jeshi hilo jambo ambalo ni udanganyifu.

Wakati huo huo, watu wanne wanashikiliwa akiwamo mmoja kukutwa na fuvu la binadamu na wengine watatu kukutwa na ngozi ya mnyamapori na vipande vya meno ya tembo.

Kamanda Chilya alisema tukio hilo lilitokea Januari 7, mwaka huu, katika kijiji cha Naholo, Namtumbo, ambako walimkamata mwanamume mwenye umri wa miaka 47 akiwa na fuvu la kichwa cha mtu na vipande vitatu vya ngozi za wanyamapori alivyovihifadhi kwenye begi na kuvificha ndani.

Aidha, Chilya alisema katika operesheni iliyofanywa na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kanda ya Kusini, Jafari Likwata (41) mkazi wa Minazini, Nikodemas Pius Ngonyani (60) mkazi wa kijiji cha Peramiho, Songea na George Ngesala, walikamatwa wakiwa na meno ya tembo mazima 18 na vipande 11 wakiwa wameyahifadhi kwenye mfuko wa sandarusi na kuficha maeneo tofauti kwenye nyumba wanazoishi.

Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Ujangili Kanda ya Kusini, Kamishna Msaidizi Kenneth Sanga, alisema meno hayo yana uzito wa kilogramu 43.8 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500.3 na vipande 11 vya zaidi ya Sh. milioni 201.6

Kamanda Chilya alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani mara baada ya upelelezi kukamilika.

# DC akalia kuti kavu kutukana wananchi

**Beatrice Shayo, aliyekuwa**
SIMIYU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kuna mkuu wa wilaya aliyepewa maagizo kuwa mwananchi aliyeshinda kesi ya ardhi anapatiwa haki yake lakini amemnyang'anya nyaraka zake na kumtukana.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu.

Makonda alisema mikutano wanayoifanya si ya maigizo na maagizo wanayoyatoa kwa viongozi wanatakiwa kuyatekeleza na si kufanywa kinyume.

"Tumepita wilaya moja mtu ameshinda kesi yake na kwenye timu tuliyo nayo tuna timu ya wanasheria. Tukampa jukumu mkuu wa wilaya ahakikishe anakwenda na huyo mwananchi akamkabidhi eneo lake kwa sababu alishinda kesi.

"Baada ya kutoka katika wilaya hiyo, mkuu wa wilaya alijua kwa kuwa tumeondoka hakuna atakayewapatia taarifa. Kamnyang'anya karatasi yule mwananchi na kumpa matusi ya ajabu kwa kuamini ya kwamba tulivyoondoka hatutajua kinachoendelea lakini taarifa zake tunazo," alisema. Makonda alisema hatatumia cheo chake kujinufaisha lakini wako baadhi ya watendaji si waaminifu wanaosababisha wananchi kukosa haki zao.

"Nikikukabidhi jambo chonde chonde usidhani kwa vile tumeondoka limeishia hapo. Tunafuatilia yakija kukukuta usije kusema fulani kaniharibia. Tutakuharibia kweli kwa kuwa na wewe una mpango wa kutuharibia mwaka 2025 hatutakubali utupotezee kura na wala kumchonganisha Rais wetu na wananchi wake,"alisema.

Aidha, Makonda alisema wanaouliza kwa nini anahoji viongozi wa serikali kazi yao wanatafuta majungu na jukumu lake kubwa ni kuhakikisha Rais Samia anapata ushindi wa kishindo mwaka 2025.

Makonda alisema wana kiongozi ambaye hana kisasi wala makundi shida ipo kwa wapambe ambao wanafanya uharibifu kwa wenzao kwa kupeleka majungu.

Alisema bila CCM madhubuti taifa litayumba na kwenye katiba ya CCM ya mwaka 1977 iliyofanyiwa mabadiliko mwaka 2022 kwenye sura ya utangulizi, waasisi walipokuwa wanaanzisha chama hicho, walieleza wanaunganisha TANU na ASP ili kutokomeza unyonyaji, unyanyasaji na ukandamizaji.

Alisema wakiunda serikali ina maana wamefungua duka na kazi yao kuuza bidhaa, hivyo yeye anapita kukagua je muuzaji wao anauza vizuri na kama wateja wanapungua wanamhoji kwa nini mauzo yanashuka.

Aidha, Makonda alisema Rais Samia ana dhamira njema ya kuwatumikia Watanzania na kuwaletea maendeleo ndio maana amekuwa akitoa mabilioni ya fedha kutekeleza miradi.

Makonda aliwaomba Watanzania kuendelea kumuombea Rais Samia na kumuamini katika jitihada zake mbalimbali anazozifanya ikiwemo kutafuta na kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kutafuta soko la mawazo ya biashara nje ya nchi.



Balozi wa Uturuki nchini, Mehmet Güllüoğlu (kushoto), akikabidhi sehemu ya msaada wa vitu mbalimbali uliofadhiliwa na Hilali Nyekundu ya Uturuki (Turkish Red Crescent) kwa Mkuu wa Wilaya ya Manyara, Janet Mayanja, kwa ajili ya waathirika wa mafuriko wilayani Hanang, Mkoa wa Manyara juzi. Wa pili kushoto ni Katibu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Lucia Pande na Rais wa chama hicho, David Kihenzile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madeni ya bil. 981.8/- yafutwa kisa nyaraka

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imefuta madeni ya Sh.bilioni 981.79 kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo kukosekana kwa nyaraka, baadhi kubainika kulipwa tayari na makosa ya ukokotoaji.

Hayo yalibainishwa jana bungeni jijini hapa baada ya wabunge kuhoji serikali kuhusu mkakati wa kulipa madeni ya wazabuni na makandarasi wa ndani kutokana na baadhi yao kufilisiwa na benki zilizowapa mikopo.

Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, alihoji serikali imelipa au kukataa madeni mangapi ya wazabuni na makandarasi wa ndani tangu ianze uhakiki kwa kuwa ni ya muda mrefu.

Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo alihoji sababu za serikali kuchelewesha malipo kwa makandarasi wazawa ambao wamekamilisha miradi.

Aidha, Mbunge wa Mbulu Mjini (CCM), Zacharia Isaay, alihoji mkakati wa serikali wa kulipa makandarasi kwa wakati.

Kutokana na maswali hayo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali kwakutambua umuhimu na mchango wa sekta binafsi katika maendeleo na uchumi wa taifa, imeendelea kutenga na kulipa madeni ya wazabuni na makandarasi yaliyohakikiwa na kukubaliwa.

Aidha, alisema serikali imeongeza bajeti ya madeni kutoka wastani wa Sh. bilioni 400 hadi Sh.bilioni 700.00 kwa mwaka.

"Katika kipindi cha mwaka 2014/15 hadi Desemba 2023, madeni ya wazabuni na makandarasi yaliyowasilishwa kwa uhakiki yalikuwa zaidi ya Sh. trilioni 3.1. kati ya kiasi hicho, yaliyolipwa ni zaidi ya Sh. trilioni 2.128.54 na zaidi ya Sh.Trilioni 1.03 ni madeni ya wazabuni na zaidi ya Sh.Trilioni 1.09 ni madeni ya makandarasi,"alisema.

Kuhusu ucheleweshaji malipo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, alisema Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha zimekuwa zikishirikiana kuhusu upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na kulipa madai na madeni ya makandarasi.

Alisema malipo kwa makandarasi wote nchini hufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

Pia alisema makandarasi wazawa wamekuwa wakipewa kipaumbele katika malipo pindi fedha zinapotolewa.

# NMB yaweka rekodi mpya ikipata faida ya bil. 775/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeweka rekodi mpya ya ufanisi kiutendaji kwa kutengeza faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 775 na kupata mafanikio mengine kifedha ambayo uongozi wake umesema yamechangia kubadilisha maisha ya watu na kuwa na tija katika uchumi wa taifa.

Akitangaza matokeo ya mafanikio hayo ya kihistoria jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, aliwaambia waandishi wa habari kuwa rekodi mpya ya faida imetokana na ukuaji mkubwa wa mikopo, kuongezeka kwa wateja na miamala pamoja na amana, ubora wa mikopo na kiwango cha juu cha ufanisi.

Alibainisha kuwa faida hiyo kubwa imepatikana baada ya jumla ya mapato ya mwaka 2023 kufikia Sh. trilioni 1.4 kutokana na ukuaji wa asilimia 24 wa mapato ya riba na asilimia 15 ya mapato yasiyotokana na riba.

"Kutokana na ufanisi huu, faida kabla ya kodi imeongezeka kwa asilimia 26 hadi Sh. bilioni 775 huku faida baada ya kodi ikifika Sh. bilioni 542 ikiwa ni ongezeko la asilimia 26 kwa mwaka. Hiki ni kiwango kikubwa cha faida na cha kihistoria kwa benki ya NMB na sekta nzima ya fedha nchini," Zaipuna alisema.

Katika kuonesha ukubwa wa ukuaji huo, kiongozi huyo alibainisha kuwa mwaka 2020 wakati NMB inaweka Mpango Mkakati wa Muda wa Kati (2021-2025), jumla ya mapato ilikuwa Sh. bilioni 842, huku faida kabla ya kodi na baada ya kodi zikiwa Sh. bilioni 296 na Sh. bilioni 206 mtawalia.

"Mizania ya benki imeendelea kukua na kufikia jumla ya mali ya Sh. trilioni 12.2 ikiwa ni ukuaji wa asilimia 19 kwa mwaka, huku ukwasi na mtaji wa benki ukiwa imara na juu ya viwango vya Benki Kuu.

"Ukuaji huu ulitokana hasa na kukua kwa amana za wateja kwa asilimia 12 pamoja na ongezeko la mikopo la asilimia 28," aliongeza.

Alisema ufanisi mkubwa kwenye gharama za uendeshaji na ubora wa mikopo ulitokana na kuboreshwa zaidi kwa uwiano wa gharama za uendeshaji na mapato kufikia hadi asilimia 39, wakati uwiano wa mikopo chechefu ulishuka hadi asilimia 3.2, viwango ambavyo ni chini ya ukomo wa kikanuni wa Benki Kuu wa asilimia 55 na asilimia tano mtawalia.

"Tunajivunia ufanisi mkubwa na matokeo chanya ya kiutendaji yaliyopatikana katika maeneo muhimu ya utekelezaji mkakati wetu, ikiwamo ujumuishwaji wa watanzania kwenye sekta rasmi ya kifedha, utoaji huduma bora kwa wateja na uwekezaji wa kimkakati kwa wafanyakazi wetu, utawala bora na uwekezaji kwenye teknolojia ili kuongeza thamani," Zaipuna alibainisha.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa ufanisi na matokeo haya ya kiutendaji umekuwa pia na matokeo chanya hata kwenye bei ya hisa za NMB ambayo iliongezeka kwa asilimia 49 kutoka Sh. 3,020 hadi kufikia Sh. 4,500 kati ya Januari na Desemba 2023.

Alisema ongezeko hilo la bei ya hisa limefanya mtaji wa Benki ya NMB kwenye soko la hisa kufikia Sh. trilioni 2.25 kutoka Sh. trilioni 1.5 za Desemba 2022.

"Hili limepelekea NMB kuwa benki kubwa zaidi iliyoorodheshwa kwenye soko la hisa Tanzania na masoko yote ya hisa Afrika Mashariki kwa kigezo cha thamani ya kampuni kwenye soko la hisa 'market capitalization'.

"NMB kwa sasa ni kampuni ya nne kwa ukubwa kwa kampuni zilizoorodheshwa Afrika Mashariki, baada ya Safaricom ya Kenya, Tanzania Breweries na MTN-Uganda na ni ya 26 kwa ukubwa kati ya kampuni zilizoorodheshwa Kusini mwa Jangwa la Sahara (ukiondoa Afrika Kusini)," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa hiyo ni mara ya kwanza kwa NMB kuwa katika orodha hiyo na kuwa benki pekee ya Tanzania kuwahi kuingia kwenye orodha ya kampuni 30 kubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Mafanikio yaliyopatikana mwaka 2023 yanaonesha jukumu la NMB kuendelea kuwa injini ya ustawi wa kiuchumi nchini na mwezeshaji wa kuzifungua fursa mpya kwa wateja na wadau wetu wote Tanzania," Zaipuna alitamba.

Alisema kwa mwaka 2024, NMB itaendelea kurahisisha upatikanaji huduma za kibenki nchini hasa vijijini na maeneo yaliyo pembezoni na hivyo kuongeza ujumuishwaji wa watanzania wengi kwenye sekta rasmi ya kibenki kupitia suluhisho bunifu kama NMB Pesa.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Juma Kimori, alisema ufanisi wa mwaka jana ni ishara ya nidhamu na umakini katika kutekeleza kwao Mpango Mkakati wa Muda wa Kati ambao moja ya malengo yake ni kuhakikisha NMB inaendelea kuwa mbia nambari moja wa serikali na jamii nzima ya watanzania katika kuchagiza maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

TANGAZO

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Disemba-2023 | Robo Mwaka iliyopita 30-Septemba-2023 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 708 | 617 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 6,843 | 14,576 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 63 | 54 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 9 | (53) |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 7,372 | 6,371 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 62,476 | 61,859 |
| 12. Mali Nyingine | 2,555 | 2,050 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,057 | 962 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **81,083** | **86,436** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | 2,400 | 4,038 |
| 18. Amana za Wateja | 58,709 | 59,320 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,503 | 1,844 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 607 | 3,287 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27. Dhima Nyingine | 1,213 | 2,433 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **65,432** | **70,922** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,651** | **15,514** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 17 | 17 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (20,302) | (20,302) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 24 | (114) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,651** | **15,513** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 1,111 | 1,200 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (601) | (592) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 19.3% | 17.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.8% | 1.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 101.3% | 96.7% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 76.3% | 70.9% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 86.1% | 78.9% |
| - Ongezeko la Amana | -3.6% | -6.1% |
| - Ongezeko la Mali | -6.2% | -2.4% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 31-Disemba-2023 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Disemba-2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Disemba-2023 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Disemba-2022 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 2,574 | 2,538 | 10,285 | 8,641 |
| 2. Gharama za Riba | 1,193 | 879 | 4,580 | 3,192 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,381** | **1,659** | **5,705** | **5,449** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 77 | 45 | 283 | 45 |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 582 | 480 | 1,915 | 1,996 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | - | - | (8) | 5 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 537 | 367 | 1,696 | 1,771 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 45 | 113 | 227 | 220 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,710 | 2,027 | 7,240 | 7,304 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 651 | 755 | 3,028 | 3,113 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 1,059 | 1,272 | 4,212 | 4,191 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **176** | **67** | **97** | **96** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (40) | (15) | (74) | (15) |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **136** | **52** | **23** | **81** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **136** | **52** | **23** | **81** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 67 | 58 | 67 | 58 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 3 | 1 | 2 | 2 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *0.2%* | *0.1%* | *0.0%* | *0.1%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *0.9%* | *0.3%* | *0.2%* | *0.5%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *87.0%* | *94.8%* | *95.0%* | *98.1%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2.0%* | *2.4%* | *8.2%* | *7.8%* |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2023 (Kias kwa shilingi milioni)i | Robo Mwaka ya sasa 31-Disemba-2023 | Robo Mwaka iliyopita 30-Septemba-2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Disemba-2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Disemba-2022 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | 233 | (136) | 97 | 96 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 453 | 496 | 949 | 1,244 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,790 | (5,408) | (1,618) | (23,944) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (3,514) | (2,903) | (611) | 21,459 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (3,168) | 73 | (3,241) | 3,670 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,762) | 2,544 | (218) | (221) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | (34) | - |
| - Mengineyo | 5 | 65 | 70 | (300) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(4,963)** | **(5,269)** | **(4,606)** | **2,004** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (89) | (120) | (209) | (229) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(89)** | **(120)** | **(209)** | **(229)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,951) | (5,421) | (4,815) | 1,775 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,424 | 10,845 | 5,424 | 6,051 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3,473 | 5,424 | 609 | 7,826 |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2023**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ........................ (Imesainiwa) | 29 Januari 2024 |
| Maulid M. Tarimo (Kaimu Mkuu wa Fedha) | ........................ (Imesainiwa) | 29 Januari 2024 |
| Joanitha Mashulano (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ........................ (Imesainiwa) | 29 Januari 2024 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ........................ (Imesainiwa) | 29 Januari 2024 |
| 2/ Berthasia L Patrick (Mkurugenzi) | ........................ (Imesainiwa) | 29 Januari 2024 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mtaji Tangulizi | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (20,254) | 5,000 | - | 15,658 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 23 | | - | 23 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | - | | 17 | 17 |
| Mengineyo | - | (48) | | - | (48) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30.912** | **(20.279)** | **5.000** | **17** | **15.650** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | - | 16,017 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | (331) | | | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | (17) | | 17 | |
| Mengineyo | - | (11) | | - | (11) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,254)** | **5,000** | **17** | **15,675** |

MCB BANK BETTER TOGETHER
Mwalimu Commercial Bank Plc
Ada
Chap Chap
Mkopo wa haraka kwa ajili ya ada ya shule kwa waajiriwa wanaotaka kujiendeleza kielimu au kwa ajili ya kulipa ada za wategemezi wao



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari zaidi zichukuliwe dhidi ya mvua inayoendelea

**MVUA** inaendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini huku maafa katika baadhi ya sehemu yakitajwa kutokea. Miongoni mwa maafa hayo ni vifo vya watu, uharibifu wa miundombinu na mali yakiwamo makazi.

Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari na taasisi za serikali, katika baadhi ya maeneo watu wamepoteza maisha baada ya mvua kubwa kunyesha na kuvamia makazi ya watu.

Pia kwenye baadhi ya maeneo, imebainishwa kuwa mvua imeharibu miundombinu ya usafirishaji kama vile reli na barabara, hivyo kusababisha watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine kushindwa kusafiri. Licha ya kusababisha tatizo hilo, baadhi ya maeneo, kama vile ilivyoripotiwa kwenye barabara kuu ya Morogoro - Dodoma, maji yamejaa barabarani, hivyo magari kusimama kwa muda kabla ya kupungua kwa maji kisha kuendelea na safari.

Taarifa zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) zinabainisha kuwa mvua hiyo ambayo ilianza tangu mwishoni mwa mwaka jana itaendelea kunyesha, hivyo maeneo mengi kupata athari mbalimbali ikiwamo miundombinu kuharibika hata kutokea kwa maafa katika sehemu za makazi.

Katika mkoa wa Dar es Salaam, baadhi ya maeneo yameendelea kuathirika hususani watu waliojenga maeneo ya bondeni. Katika maeneo hayo imeshuhudiwa nyumba zikiingiliwa na maji ya mvua, maji kuharibu barabara huku baadhi ya sehemu kukitokea vifo.

Aidha, baadhi ya nyumba ambazo ziko kwenye miinuko na maeneo yenye asili ya kufurika maji kila mvua inyeshapo, yameanza kupata athari, ikiwamo nyumba kuanza kuonyesha dalili za kubomoka.

Hali hiyo ni ishara kwamba kuna madhara makubwa yanayotarajiwa kutokea kutokana na mvua kuendelea kunyesha kwenye sehemu mbalimbali za nchi, Dar es Salaam ikiwamo. Iwapo hali hiyo itaendelea kama ilivyo sasa, kulingana na utabiri wa TMA, kuna uwezekano pia wa kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko kama vile kuhara, kuhara damu na kipindupindu hatimaye kusababisha madhara kwa baadhi ya wananchi.

Kuna msemo kwamba tahadhari kabla ya hatari, hivyo ni vyema jitihada zaidi za kukabiliana na maafa hayo ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Miongoni mwa tahadhari zinazoweza kuchukuliwa ni kuzibua mifereji ya maji mbayo imeziba kutokana na kuwa na takataka nyingi, husababisha maji kutokusafiri katika mikondo husika hivyo kujaa na kusambaa kwenye makazi ya watu.

Katika baadhi ya sehemu hasa barabara ambazo zinasababisha maji kujaa barabarani na kusababisha usafiri kuwa na changamoto, ni wakati mwafaka kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kutafuta suluhisho la kudumu.

Maeneo hayo, si mara ya kwanza kukumbwa na adha hiyo, ndiyo maana inasisitizwa kuwa taasisi hizo zenye dhamana ya kusimamia barabara kuchukua hatua na kumaliza tatizo hilo. Pia kuna jambo la kujifunza kuhusu madhara yatokanayo na athari mbalimbali kama vile mvua wakati wa ujenzi wa miundombinu hiyo.

Pamoja na wakala wa barabara kuchukua hatua, wananchi wanapaswa kufanya usafi wa mifereji na kuruhusu maji kupita kwenye mikondo yake baada ya kuyazuia na kufanya sehemu hizo kukumbwa na madhara yatokanayo na mvua.

Ni imani kwamba kama tahadhari zitachukuliwa na mambo mbalimbali kufanyiwa kazi katika kukabiliana na maafa, madhara yatokanayo na mvua yatapungua, hivyo wananchi kuishi kwa amani na utulivu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Uanze mfumo kudhibiti wasio raia kuwa viongozi

**UTOAJI** wa vyeti vya kuzaliwa unatajwa kuwa ni kichocheo kwa wakimbizi kupata nyaraka hizo kirahisi na kuwafanya baadhi yao kuajiriwa serikalini.

Ajira yao ni jambo linaloelezwa kuwa si jema kiusalama, kutokana na ukweli kuwa hakuna anayejua malengo ya wageni hao kujiingiza serikalini.

Katika mkutano wa makamanda wa Jeshi la Wananchi unaofanyika hivi karibuni Dar es Salaam, Mkuu wa Majeshi (CDF), Jenerali Jacob Mkunda, anadokeza kuwa kuna baadhi ya waomba hifadhi na wakimbizi wameajiriwa katika nafasi mbalimbali serikalini.

Anafafanua kuwa kuwapo kwa ajira hizo ni kitisho kwa usalama, kauli ambayo nadhani inatakiwa kuchukuliwa kwa uzito na kutafutwa njia ya kubuni mfumo usiokuwa na mianya hiyo ili kulilinda taifa.

Labda tukumbuke kuwa wakati wa utawala wa chama kimoja, serikali iliweka utaratibu ulioshirikisha wananchi kuanzia ngazi ya chini hadi juu kwa kuwajumuisha wa nyumba 10 kwenye utambuzi wa wageni.

Wajumbe hao walikuwa na majukumu mengi yakiwamo ya kukusanya taarifa mbalimbali, ambayo yalilenga kutambua wageni na wenyeji kwenye himaya zao, kwa ajili ya usalama wa maeneo yao.

Enzi hizo, mjumbe wa nyumba 10 au balozi aliwafahamu watu wote waliokuwa wanaishi katika nyumba hizo na hata ulinzi wa sungusungu ulikuwa unafanyika katika misingi ya nyumba 10 kumi.

Vilevile kila mtoto aliyezaliwa ilibidi kwanza aandikishwe kwa mjumbe na hata vyeti vya kuzaliwa kulikuwa na nafasi ya kujaza jina la mjumbe ikiwa ni eneo la kuonyesha umuhimu katika jamii.

Aidha, pale mtu alipofariki, ilibidi pia mjumbe awe na taarifa, mgeni yoyote akiingia kwenye kaya , ilikuwa ni lazima akatambulishwe kwa mjumbe, anatoka wapi amekuja kwa ajili gani na atakaa muda gani.

Kwa ujumla kuwapo kwa wajaumbe hao kulikuwa na faida nyingi kwa jamii na taifa hasa usalama wa raia ulikuwa imara zaidi, ujambazi kupungua na usalama kuwa suala la kipaumbele.

Baada ya mfumo wa vyama vingi kurejeshwa, sasa muundo wa uongozi unaotumika ni wa serikali za mitaa, hivyo uzito wa wajumbe wa nyumba 10 waliopo sasa sio kama wa enzi hizo.

Tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi, mabalozi wa nyumba 10 ambao walipatikana katika mashina, hawana mamlaka yoyote kisheria.

Lakini tutakubaliana kuwa walifanya kazi kubwa ndani ya jamii mijini na vijijini.

Ninaamini kwamba kutokuwapo kwao, kumeacha ombwe ambalo linasababisha baadhi ya mambo kwenda ndivyo sivyo katika maeneo mbalimbali mitaani ambayo yanalalamikiwa.

Wajumbe wa nyumba 10 wapo kwa jina hilo, lakini unakuta mmoja anaongoza hata nyumba 50, lakini hana madaraka kama ya zamani, badala yake wapo wajumbe wa serikali za mitaa ambao ni wachache.

Si vibaya ujumbe wa nyumba 10 ukawa ni ngazi ya kiserikali kwani uwapo wao enzi hizo, ulinzi na usalama wa maisha na mali za watu ulikuwapo na ilikuwa ni nadra kusikia mfululizo wa matukio ya kihalifu.

Iwapo utatafutwa mfumo ambao unafanana na huo wa wajumbe wa nyumba kumi, ninaamini hata hilo tatizo alilosema CDF linaweza kudhibitwa kirahisi katika maeneo mbalimbali.

Kwa sasa imekuwa ni jambo la kawaida kuona wageni wanafika katika nyumba za watu bila hata kuulizwa wanatoka wapi, watu wanahama moja kwenda kupanga nyingine bila kuulizwa ni akina nani.

Katika mazingira hayo pia kuna wahalifu, madanguro, magenge ya kuuza biadhaa haramu lakini hakuna anayewafikia na kuwaripoti.

Uhalifu unaendelea na baada ya kumalizana na wenye nyumba, si rahisi kutambua kama ni wageni kutoka nje ya nchi au ni wa wahalifu na hivyo kuhatarisha usalama kama inavyoelezwa.

Ikumbukwe kuwa wajumbe wa nyumba kumi wa sawa wanaongoza maeneo makubwa lakini hawana nguvu kama zamani, lakini pia wajumbe wa serikali za mitaa nao ni wachache hawafanyi kazi kama ilivyokuwa kwa wajumbe wa nyumba kumi wa enzi hizo.

Kwa mantiki hiyo, ninadhani ipo haja ya kubuni mfumo utakaowafanya wajumbe wa nyumba kumi wa sasa kufanya kazi waliokuwa wakiifanya zamani ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

HABARI KITAIFA

# Serikali yakamilisha mwongozo ajira kwa vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekamilisha mwongozo wa ajira kwa vijana wanaojitolea kwenye sekta mbalimbali na kuahidi kutoa taarifa yake bungeni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alibainisha hayo jana bungeni baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson kuhoji kuhusu mwongozo huo kama umekamilika au bado.

Spika Tulia alisema; "Tunausubiri sana huo mwongozo maana vijana wanaojitolea huko kwenye sekta nyingi wako wengi."

Akitoa majibu ya suala hilo, Simbachawene alisema; "Tunaendelea lakini tumeshamaliza na tutakuja kutoa tamko hapa bungeni."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga, alitaka kujua utaratibu unaotumika kuajiri watendaji kwenye halmashauri nchini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Festo Dugange, alisema utaratibu unaotumika kuajiri maofisa watendaji wa vijiji/mitaa na kata ni mamlaka za serikali za mitaa kutenga fedha za mishahara kwenye bajeti na kuomba kibali cha ajira Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora baada ya kupata kibali Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekasimiwa jukumu la kutangaza, kuwafanyia usaili waombaji, kuwaajiri na kuwapangia vituo vya kazi maofisa watendaji waliokidhi vigezo vya ajira," alisema.

Alisema utaratibu huo unashirikisha halmashauri na mamlaka za ajira za serikali kuu.

"Katika kipindi cha miaka ya fedha ya 2020/21 hadi 2022/23 serikali imeajiri maofisa watendaji wa vijiji na mitaa 1,659 na maofisa watendaji wa kata 394 na kuwapanga kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na mahitaji," alisema.

Aidha, alisema serikali itaendelea kutenga bajeti na kutoa vibali vya ajira kwa maofisa watendaji wa vijiji/mitaa na kata kulingana na mahitaji kote nchini.




Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Suleiman Msangi (kulia), akimhudumia mwanachama aliyetembelea banda la mfuko huo, katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# NHC kujenga majengo kisasa kwa ubia na kampuni 21

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Nyumba (NHC), limesaini mikataba na wabia 21 ambao watajenga majengo ya kupangisha na ya biashara kwenye maeneo yanayomilikiwa na shirika hilo.

Makubaliano hayo yalisainiwa jana jijini Dar es Salaam na kushuhudiwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa.

Aliipongeza NHC kwa mageuzi hayo makubwa kwa kuwa ujenzi utakapokamilika kutaongeza idadi ya wapangaji kutoka 190 mpaka 2011.

Alisema kwenye maeneo hayo kwa sasa kuna nyumba 72, lakini baada ya ujenzi zitaongezeka na kuwa 225 ikiwa ni mara tatu na nusu ya zilizoko sasa na kuwataka kuwapa kipaumbele wapangaji waliokuwa kwenye nyumba hizo baada ya kukamilika kwa ujenzi wa majengo mapya.

"Nafahamu kuwa mmeshaanza kuchukua hatua kwa kuwanyang'anya wabia waliolegalega katika mikoa ya Arusha, Morogoro na Dar es Salaam. Huu ni uamuzi sahihi na endeleeni kuitwaa miradi yote iliyosimama ili muiendeleze iweze kuleta tija kwa shirika na taifa letu," alisema.

"Kadhalika, natambua kuwa bado kuna miradi ya ubia ya zamani ambayo inaendelea kukamilishwa kwa hiyo hakikisheni mnaisimamia kikamilifu ili nayo iweze kukamilika mapema iwezekanavyo," alisema Waziri.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdalah Hamad, alisema shughuli za ujenzi zinatarajia kuanza mwezi wa pili kwa majengo 16 kubomolewa baada ya wapangaji kupewa notisi ya kuondoka.

Alisema baada ya kutangaza maeneo uendelezaji wamepokea maombi 59 ya kuendeleza viwanja 28 na kuchambuliwa kwa kuzingatia vigezo tisa vilivyowekwa ambavyo ni barua ya maombi, andiko la mradi, dhana, gharama na wasifu wa kampuni.

Alitaja vigezo vingine kuwa ni nyaraka za usajili wa kampuni, uwezo wa kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, taarifa za kifedha zilizokaguliwa pamoja na ujuzi na uzoefu wa kampuni katika utekelezaji wa miradi ya uendelezaji milki kuu.

Alisema baada ya uchambuzi na tathmini ya kina, jumla ya waleta maombi 24 walipendekezwa kwa ajili ya kuidhinishwa na Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika.

Hamad alisema bodi iliidhinisha maombi hayo 24 na baada ya kuendelea kuchambua kwa kupitia vigezo vyote muhimu, miradi mitatu imeondolewa kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo wabia kushindwa kuendelea na nia yao ya kuendelea na utekelezaji wa miradi.

Alisema miradi 21 iliyopitishwa inajumuisha viwanja 16 vilivyopo Kariakoo, kiwanja kimoja kilichopo Upanga, viwanja viwili vilivyopo jijini Mwanza na mradi mmoja kwa kiwanja kilichopo Iringa.

"Miradi yote hii 21 iliyoidhinishwa ina thamani ya jumla ya takribani Sh. bilioni 271 ikilinganishwa na thamani ya sasa ya majengo hayo ambayo ni bilioni 59," alisema.

Alisema miradi inayotarajiwa kutekelezwa itaongeza idadi ya nyumba za kuishi pamoja na maeneo ya biashara na kuchangia kutatua changamoto ya makazi bora na maeneo bora ya kibiashara.

Alisema miradi inayotarajiwa kutekelezwa eneo la Kariakoo itakuwa na jumla ya wapangaji 2,011 (maduka 1,258 stoo 500 na nyumba za makazi 253 ikilinganishwa na idadi ya sasa ambayo ni wapangaji 190.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza mwezi Februari 2024. Miradi yote inatarajiwa kuchukua muda wa miaka miwili hadi mitatu kukamilika kulingana na ukubwa wa kila mradi.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Watumishi 51 wachukuliwa hatua matumizi mabaya fedha za miradi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Desemba 2023, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilianzisha uchunguzi kwa miradi 274 na watumishi 51 walichukuliwa hatua za kinidhamu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbogwe (CCM), Nicodemas Maganga, aliyetaka kujua serikali inachukua hatua gani kwa watumishi wanaohusika na kutumia vibaya fedha za miradi ya serikali.


Alisema kwa kipindi hicho TAKUKURU ilifuatilia matumizi ya rasilimali za umma kwenye utekelezaji wa miradi 2,541 yenye thamani ya Sh. trillioni 8.26 na miradi 467 ilibainika kuwa na upungufu ikiwamo ufujaji na kutokuwa na thamani ya fedha.

Alisema hatua kadhaa zilichukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329, ikiwa ni pamoja na kuanzisha uchunguzi kwa miradi 274 watumishi 51 walichukuliwa hatua za kinidhamu.

Alibainisha kuwa usimamizi wa masuala ya nidhamu katika utumishi wa umma huzingatia matakwa ya kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 ambacho kimewapa mamlaka wakuu wa taasisi kusimamia masuala ya nidhamu kwa watumishi walio chini yao wanapokiuka kiapo cha ahadi ya uadilifu.

"Katika kuzuia uvunjifu wa maadili katika utekelezaji wa majukumu ikiwamo wa miradi ya maendeleo, serikali imeendelea kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wa umma wanaotumia vibaya fedha za miradi ya maendeleo ikiwamo kuwasimamisha kazi na kuwaanzishia mashauri ya kinidhamu," alisema.

Alisisitiza ofisi hiyo itaendelea kufuatilia utekelezaji wa sheria na kanuni ili watumishi wa umma wazingatie miiko na maadili ya utumishi wanapotekeleza miradi ya maendeleo pamoja majukumu mengine katika ofisi za umma.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe (kulia), akizungumza na wajenzi wa Kituo cha RAFIC kilichoko katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Kampasi Kuu jijini Dar es Salaam alipotembelea ili kuona maendeleo yake, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Bil. 1/- yatolewa kudhibiti matumizi ya kuni gerezani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetoka Sh. bilioni moja ili kuwezesha matumizi ya nishati safi badala ya kuni wakati wa kupika chakula kwa ajili ya wafungwa na mahabusu katika vituo 19 vya magereza nchini.

Mkurugenzi wa Rasilimaliwatu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mariam Mbaga, alibainisha hayo wakati wa uzinduzi wa upandaji miti katika eneo la Veyula, mkoani Dodoma.

Alisema lengo lao ni kudhibiti uharibifu wa mazingira unaofanywa ili kupata kuni kwa ajili ya kupika chakula cha wafungwa.

"Serikali inapambana kuhakikisha nishati safi inatumika katika magereza mbalimbali nchini. Lengo lao ni kuona nishati safi inatumika kwa ajili ya matumizi ya kupikia chakula cha wafungwa katika magereza yetu," alisema.

Akizungumzia upandaji miti, Mariam alisema mwaka jana walipanda miti mingi na wanatarajia kupanda miti milioni 700 katika maeneo mbalimbali nchini. Wanaunga mkono jitihada za serikali kulinda mazingira.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shakimweri, alisema Jeshi la Magereza wanastahili pongezi kutokana na upandaji miti wanaofanya kila mara.

Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Magereza, Kamishna Ramadhan Nyamka, SACP Salum Onary ambaye ni Kaimu Kamishna wa Huduma za Urekebu wa Jeshi la Magereza, alisema suala la upandaji miti kwa magereza ni jambo la kawaida kwao na ni utaratibu ambao wamejiwekea.

Alisema miti hiyo itaangaliwa vizuri ikiwamo kumwagiliwa ili istawi kwa ajili ya kuleta kivuli na matunda.

**Alisema lengo lao ni kudhibiti uharibifu wa mazingira unaofanywa ili kupata kuni kwa ajili ya kupika chakula cha wafungwa.**

# TBS yawapa angalizo waagizaji vyakula, vipodozi

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Nchini (TBS), limewataka wafanyabiashara wa vyakula na vipodozi vinavyotoka nje ya nchi kuwasilisha sampuli kupimwa na shirika kabla ya kuingiza sokoni.

Ofisa Ukaguzi wa (TBS), Adamu Mitumba, alisema hayo jana katika Maonesho ya Ghana EXPO Tanzania 2024 yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

"Bidhaa za vipodozi na vyakula zinahitaji ziwe na usajili kutoka TBS, kama mfanyabiashara anasafirisha bidhaa hizo kutoka nje anatakiwa kuwasilisha sampuli ya bidhaa hizo ili kupimwa na kama zinakidhi viwango ndipo ataruhusiwa kuleta hiyo shehena na kwa bidhaa ambazo si za chakula wanatakiwa kutumia mawakala wetu katika kanda husika," alisema Mitumba.

Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alisema shirika limetoa elimu kwa umma na wafanyabiashara katika maonesho hayo yenye lengo la kujenga ufahamu wa majukumu ya taasisi hiyo kwa wageni kutoka nchini Ghana na wenyeji kuhusu utaratibu wa kuingiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Alisema wametoa elimu kwa wageni kutoka nchi ya Ghana ambao wengi waliuliza kuhusu taratibu za uingizaji wa bidhaa nchini ili kukidhi matakwa ya viwango vya Tanzania.

"Elimu hiyo imetolewa kwa washiriki na wengi wameishukuru TBS, kwani hata walipoleta bidhaa zao kwa ajili ya maonesho walipata huduma nzuri bila usumbufu wowote," alisema Mayugu.

Aidha, alisema wenyeji waliofika katika banda la TBS walielezwa kuhusu taratibu za kupata alama ya ubora ambayo itawasaidia kutanua wigo wa kukuza bidhaa zao katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Pia wametoa elimu kwa wananchi waliotembelea maonesho hayo waliotaka kujifunza kuhusu maelezo ya msingi yanayopatikana katika bidhaa ambazo zinakidhi viwango kwa ajili ya matumizi.

Vilevile, Mayugu aliwataka watumiaji wa bidhaa nchini kusoma maelezo yanayopatikana katika vifungashio vya bidhaa ili kutambua muda wa matumizi na alama ya ubora ili wawe na uhakika na usalama wa bidhaa husika.

Aidha, Mayugu alitoa wito kwa wazalishaji na waagizaji wa bidhaa nchini, kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango kwa matumizi ya binadamu.



## Watakiwa kuimarisha uhai wa chama

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Loy Ole Sabaya amewataka viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi ya mashina hadi wilaya kufanya vikao ili kuimarisha uhai wa chama kuelekea uchaguzi wa serikali na mkuu mwakani.

Sabaya, pia amewaonya wanachama wa CCM kuacha kujipitisha kwenye majimbo na kata kusaka uongozi na kuwaacha wawakilishi wa wananchi waliopo waendelee kutekeleza majukumu yao hadi watakapomaliza muda wao wa uongozi.

Akiwa katika ziara yake ya kikazi wilayani Longido juzi ya kujitambulisha na kuimarisha uhai wa chama hicho, alisema :

"Kuna vikao vingi vya kikatiba ambavyo vilikuwa havifanyiki hasa kwenye ngazi za matawi na mashina, kuanzia sasa nataka vikao vyote vya kikatiba vifanyike na mihutasari wa kila kikao uwasilishwe ngazi husika."

Aliwataka viongozi wa kata na matawi kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ya mwaka 2020/2025 katika maeneo yao na kufanya mikutano ya hadhara ili kusikiliza kero za wananchi.

"Ole wake kiongozi ambaye hatasikiliza kero za wananchi katika eneo lake. Ni lazima mshuke kusikiliza kero na kuzipatia majibu na muwaeleze juu ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao," alisema.

Kuhusu zuio la Noah kushusha abiria kwenye vituo vidogo hadi stendi alisema:

"Mkuu wa Wilaya haiwezekani kusiwe na vituo vidogo vya kushusha abiria na kuwalazimisha washuke stendi. Kama ni mapato mnahitaji Noah zipite stendi zilipe ushuru, lakini abiria washuke kwenye vituo vidogo."

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi alisema maagizo hayo ameyapokea na atayafanyia kazi kwa kushirikiana na ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri ili wananchi waanze kupata huduma kushuka kwenye vituo hivyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Longido, Steven Ulaya, alisema halmashauri hiyo imeanza mpango wa kuboresha stendi hiyo kwa kujenga vibanda na jengo la kupumzika abiria kupitia mapato ya ndani.

Awali Ikoy Laizer, alisema serikali imepiga marufuku Noah kushusha abiria kwenye vituo vidogo na kulazimishwa hadi kwenye stendi na kusababisha usumbufu kwao.

"Mwenyekiti abiria wanaotoka Arusha kwa Noah, hawaruhusiwi kushuka kwenye vituo vidogo, wanalazimishwa kushuka stendi na huu ni utaratibu umeanza hivi karibuni unatusababishia hasara," alisema.

# Madudu fedha za miradi yahamisha watumishi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela ameamuru watumishi wawili wa Halmashauri ya Meru kuhamishiwa moja ya halmashauri za mkoa huo kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao kwenye vituo vyao vya kazi.

Mongela alitoa amri hiyo jana baada ya kukagua ujenzi wa miradi ya elimu na afya kwenye halmashauri hiyo na kubaini Shilingi milioni 150 hazikuingizwa kwenye akaunti ya Kijiji cha Oldonyong'iro na kutumika bila ya kufuata utaratibu.

Watumishi hao ni Mhasibu wa Kituo cha Afya Mareu, vituo vingine zaidi ya nane na Zahanati na mfamasia wa kituo hicho.

Mkuu huyo wa mkoa, alibaini kiasi hicho cha fedha za ruzuku zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kununua vifaa vifaa tiba hazikuingizwa kwenye akaunti ya kijiji hicho kinyume na utaratibu wa Bohari ya Dawa (MSD).

"Hapa kuna jambo kama kweli fedha hizi zimewekwa au ziko kwenye akaunti ya kijiji lazima wakati wa kutoa kungekuwapo na muhtasari wa kikao cha halmashauri ya kijiji na kuambatanishwa kwenye mchakato wa kutoa fedha za kununua vifaa tiba," alisema na kuongeza kuwa:

"Mhasibu wa kituo hiki cha afya na Mfamasia waondolewe hapa na watafutiwe halmashauri nyingine ya kuhamishiwa kwa kuwa hawatoshi na waletwe watumishi wengine wapya kwa kuwa hapa kuna madudu."

Alisema fedha zilitakiwa kuwekwa kwenye akauti ya kijiji tangu Novemba mwaka 2023, lakini hazikuwekwa kwa kuwa bado ziko halmashauri na kwamba chakushangaza zimetumika kufanya manunuzi ya vifaa hivyo.

Diwani wa Kata ya King'ori, Lucas Kaaya, alisema changamoto zilizojitokeza kwenye kituo hicho alizibaini awali na kutoa taarifa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru na ya Mkurugenzi wa halmashauri hiyo.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa tangu Novemba 29, mwaka 2023 nilikuwa hapa kufanya ziara kwenye kituo cha afya, sina taarifa yoyote ya Shilingi milioni 150 kuwekwa kwenye akaunti ya kijiji na kufikishwa kwenye kituo chetu cha afya, pia kasoro ndogo ndogo tulizobaini tuliwasilisha kwa mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ili wazirekebishe ," alisema.

Katika ziara yake hiyo, Mongela pia alikagua ujenzi wa Kituo cha Afya Mareu, vyoo wa wavulana na wasichana vya Shule ya Msingi Nashori, madarasa, choo cha walimu na jengo la utawala.

Alikagua ujenzi wa jengo la utawala katika Shule ya Sekondari ya Madira, madarasa na mradi wa maji Akeri.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini, katika viwanja vya stendi ya Bombani, mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Mashtaka wa wilaya hiyo, Petrida Mauta (kulia), Ofisa wa TAKUKURU wa Wilaya, Beatrice Alfred (wa pili kulia), Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Godfrey Haule (wa pili kushoto) na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Charles Ntenga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# REA kuwasha umeme vitongoji 54

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) wanatarajia kupeleka umeme vitongoji 54 wilayani hapa Mkoa wa Tanga katika awamu ijayo.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Mbunge wa Muheza, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (Mwana FA) wakati akizungumza na wakazi wa Kata ya Ngomeni.

Mwinjuma, alisema kati ya vitongoji 522 vya jimbo hilo la Muheza,106 vilikuwa bado havijapata umeme na kwamba kwa awamu ijayo, REA wameahidi kupeleka nishati hiyo kwenye vitongoji 54.

Alimuomba Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk.Doto Biteko kufikisha umeme kwenye vitongoji hivyo.


Katika hatua nyingine; Dk. Biteko amewasha umeme kwa mara ya kwanza kwenye nyumba ya Mzee Fredy Ndayungwa, ambao umewekwa REA katika Kijiji cha Ngomeni moja Kata ya Ngomeni Tarafa ya Ngomeni na kuahidi kumsaidia kukamilisha ujenzi wa nyumba yake.

Waziri wa Afya,Ummy Mwalimu, ameahidi kumsaidia mzee huyo kupata matibabu ya miguu kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Nyayungwa alikuwa kibarua wa Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) wakati huo ilikuwa ikijulikana kama Shirika la Reli Tanzania (TRC), akitokea mkoani Kigoma.

Mzee huyo akiwa katika utekelezaji wa majukumu yake, alipata ajali iliyopelekea kupata ulemavu wa miguu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajab Abdurrahman, alisema hadi kufikia Juni mwaka huu vitongoji vyote vitakuwa vimepata umeme.





# Polisi waomba fedha kusaidia jamii

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

JESHI la Polisi mkoani Geita limeomba kuingizwa katika orodha ya wanufaika wa fedha za huduma kwa jamii (CSR) zinazotolewa na mgodi wa Geita Gold Mine Ltd (GGML) pamoja na wawekezaji wengine mkoani hapa.

Limesema kwa kufanya hivyo litaweza kuboresha utoaji huduma bora katika jamii.

Ombi hilo lilitolewa na kamanda wa jeshi hilo mkoani hapa, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Safia Jongo wakati wa hafla iitwayo 'Police family day' iliyofanyika katika Uwanja wa Polisi mjini Geita.

Alisema kuwa fedha hizo itazisaidia Jeshi la Polisi kujenga vituo katika maeneo mbalimbali yaliyopo karibu na wananchi.

Kamanda huyo alisema hatua hiyo pia italisaidia Jeshi la Polisi kusogeza huduma ya ulinzi kwa wananchi pamoja na mali zao sambamba na kufanikisha jeshi hilo kuwa na usafiri wa uhakika ikiwemo pikipiki na magari kwa polisi wa kata.

Kadhalika aliomba ofisi hiyo kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya polisi katika kata za mkoa huo, hatua ambayo itasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao hususani katika maeneo ya migodi ambapo vurugu na matukio ya uvunjifu wa amani yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

Kuhusu 'Police family day' kamanda huyo alisema hutumika kuwambusha askari kuhusu utendaji kazi kwa kuzingatia weledi na kufanya tathimini ya kazi sambamba na kuwatunuku vyeti askari waliofanya vizuri kwa kuzingatia sheria.

Vilevile alisema siku hiyo imekuwa ikitumika kwa ajili ya kuzikutanisha familia za jeshi hilo, kuburudika na kubadilishana mawazo kwa sababu mara nyingi hawapati fursa ya kukutana na kuburudika kwa muda mrefu.

Kuhusu hali ya usalama mkoani hapa, Kamanda Jongo alisema iko salama, kwamba matukio ya uhalifu yamedhibitiwa kutokana na utendaji kazi mzuri wa maofisa wa jeshi hilo kwa kufanya kazi kwa kuzingatia weledi.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira kwa watumishi wa Jeshi la Polisi, kwamba Wilaya ya Bukombe ni moja ya wilaya ambazo zimepatiwa gari jipya.

Alisema wataendeleza ushirikiano katika kutatua kero zinazolikabili Jeshi la Polisi ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi zaidi ikiwa ni pamoja na kushirikiana na halmashauri kuhakikisha wanapata maeneo ya kujenga vituo vya polisi ili kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya mkoa.

**Limesema kwa kufanya hivyo litaweza kuboresha utoaji huduma bora katika jamii.**

# Wakulima wapewa mafunzo kuongeza thamani ya nyanya

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKULIMA wa nyanya kutoka kata za Sekebugolo na Mondo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wamepewa mafunzo ya kuongeza thamani mazao yao ili kuwaongezea kipato na kukua kiuchumi.

Mafunzo hayo yalitolewa juzi na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa Shirika la TCRS na NCA ili kuliongezea thamani zao hilo.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, Ofisa Uendeshaji Biashara kutoka SIDO Mkoa wa Shinyanga, Joseph Taban alisema mafunzo ya kuliongeza thamani zao hilo ni mkombozi kwa wakulima katika kujiongezea kipato na kuinuka kiuchumi.

"Mafunzo haya yatumieni vizuri kutengeneza bidhaa zenye ubora na kiwango cha juu ili muingie kwenye soko la ushindani wa kibiashara na kukua kiuchumi," alisema Taban.

Ofisa kutoka Shirika la TCRS, Laurent Stanslaus alisema nyanya ikiaa muda mrefu huaribika kutokana, hivyo wakalazima kuwapatia mafunzo ya kuliongezea thamani ikiwemo waweze kutengeneza tomato sosi ili wasipate hasara pamoja na kujikwamua kiuchumi.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema yatawasaidia kuwakwamua kiuchumi ikiwemo kutengeneza bidhaa zitokanazo na zao la nyanya, kutoingia kwenye hasara ya kuharibika kwa zao hilo hasa zinapokaa muda mrefu.

**Mafunzo hayo yalitolewa juzi na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa Shirika la TCRS na NCA ili kuliongezea thamani zao hilo.**



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akikata utepe na baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Simanjiro, kuzindua kampeni ya kuboresha miundombinu ya elimu, iitwayo mpe maua, atabasamu, asome kifalme, katika Mji mdogo wa Mirerani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Barrick yaboresha miundombinu shuleni kwa mabilioni

**Na Faustine Feliciane,** aliyekuwa KAHAMA

MIGODI ya Barrick ya North Mara mkoani Mara na Bulyanhulu Shinyanga imetumia zaidi ya bilioni 25 kujenga madarasa 396 na mabweni 97 katika awamu ya kwanza ya mpango wa kuboresha miundombinu ya elimu.

Migodi hiyo imepanga kutumia zaidi ya Shilingi bilioni 65 kuunga mkono juhudi za Serikali kuboresha sekta ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa 1,090 na mabweni 270 katika shule mbalimbali nchini.

Akizungumza katika mkutano wa kutoa ripoti ya robo ya nne ya mwaka iliyoishia Desemba mwaka jana, Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow, alisema awamu ya kwanza ya programu hiyo utekelezaji wake umefikia asilimia 90.

"Hii ni katika kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu, tunatarajia awamu hii ya kwanza itakamilika hivi karibu kwa kuwa imebaki asilimia 10, baada ya hapo tutaanza awamu ya pili," alisema Bristow.

Alisema mpaka kufikia Desemba mwaka jana, walikuwa wametumia shilingi bilioni 19.9 kwa ujenzi wa madarasa na mabweni hayo.

Alisema Barrick inashirikiana na TAMISEMI migodi hiyo inatoa makandarasi katika kila ujenzi ili kupata ubora wa miundombinu wanayojenga.

"Tumekuwa na ushirikiano wa karibu na wenzetu wa TAMISEMI katika kutekeleza mpango huu, tunafahamu nia na malengo ya serikali katika kuboresha sekta ya elimu hapa nchini, sisi kama wadau tutaendelea kushirikiana nao kikamilifu kufikia malengo," alisema Bristow.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema migodi hiyo imekuwa msaada kwa serikali kuleta maendeleo.

Alisema mbali na ujenzi wa madarasa na mabweni nchini, wamewezesha ujenzi wa jingo la kisasa na Uwanja wa Ndege wa Kahama.

"Kama serikali ya mkoa tunaona juhudi za wenzetu katika kuhakikisha wananchi wanafaidika na uwepo wa migodi hii, mwaka jana Wilaya ya Msalala tulipokea Shilingi bilioni 1.9 fedha za mradi wa maendeleo kwa jamii inayozunguka mgodi wa Bulyanhulu ambayo inatumika kutekeleza miradi ya maendeleo," alisema Christina na kusisitiza kuwa wataendelea kushirikiana na mgodi huo ili kuhakikisha kila mmoja anafaidika nao.

Ukurasa 13



## Maandamano ya CHADEMA ndivyo, R4 zinavyoibeba demokrasia

Ukurasa 1 4



## UCHAGUZI MAREKANI ‘Mambo yanapogeuka, msiyempenda anakuja’


# siasa

JUMATANO JANUARI 31, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


RASHID KAWAWA 1926-2009

# Mzalendo, mwanamapinduzi halisi ambaye hata sasa kazi zake zinaishi

**Na Restuta James**

NI miaka 14 sasa kuanzia Desemba 31, 2009, siku mpendwa wetu Waziri Mkuu aliyelitumikia taifa kwa uadilifu mkubwa, Rashid Kawawa, alipotwaliwa na kuiacha Tanzania aliyoshiriki kuiasisi.

Taifa linapokumbuka kifo chake. Nipashe inazungumza na wanasiasa wanaomtaja Kawawa kuwa ni taa inayotoa mwangaza wa kudumu kwa nchi japo ameondoka duniani.

“Kawawa, alikuwa mzalendo wa kweli. Alijitoa kwa ajili ya nchi yake, akiweka ubinafsi nyuma na maslahi ya taifa kwanza, hili ni jambo kubwa kuliko yote,” anasema Stephen Wasira, anapozungumzia kumbukizi za mwanamapinduzi huyo.

Wasira mwanasiasa mkongwe aliyefanyakazi na Kawawa kwani ametumikia awamu tano, anasema utumishi wake kwa umma na maisha binafsi unatafsiri namna alivyolinda maslahi ya taifa.

“Hakujitajirisha. Ukiona maisha yake na familia yake unatambua alivyokuwa mtu wa kawaida Dar es Salaam na hata nyumbani Songea alikotokea,” anafafanua Wasira.

Anamsifu Kawawa kuwa ni kiongozi wa kipekee wa kuigwa kutokana na namna alivyojitolea kutumikia Watanzania, akijituma na kuweka uzalendo na maslahi ya nchi mbele, yote yakimfanya adumu katika utumishi wa umma kwa muda mrefu pamoja na Mwalimu Julius Nyerere.

“Kawawa alikuwa mwadilifu, asiyetiliwa shaka. Alifanya kazi kwa bidii mno.Ni Mtanzania ambaye katika mazingira ya sasa hawezi kupatikana wa kufananishwa naye.

Maana tunaishi katika mazingira ambayo fedha inatawala.



Rashid Kawawa Simba wa Vita, shujaa anayeheshimika kwa makubwa aliyoifanyia Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

Watu wanaifikiria zaidi kuliko huduma au utumishi wa umma.” Anaongeza.

Anafafanua kuwa wanasiasa na wafanyakazi wa umma wanakosa sifa za Kawawa kwa kuwa wapo wachache wanaowatumikia wananchi kwa uaminifu kama wake, na kwamba kuna cha kujifunza kutoka kwake, akitaja kiwango cha juu cha uzalendo, uadilifu usiotiliwa shaka, uchapakazi na unyenyekevu.

Anamsifu kuwa akiwa kwenye utumishi wa umma, hakuchagua kazi kwa kuwa alitekeleza jukumu lolote lililompasa na kwa utendaji wake mahiri alipata jina la Simba wa Vita kutokana na uwezo wa kufanyakazi katika mazingira yote wakati wowote.

Wasira ambaye amekuwa Waziri wa Maji, Kilimo, TAMISEMI na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu), wakati wa Rais Jakaya Kikwete, anasema Kawawa alipoachiwa uwaziri mkuu na Mwalimu Nyerere, Baba wa Taifa alikiri kwamba alifanyakazi kubwa ambayo Nyerere, asingeiweza .

Miongoni mwa kazi alizofanya ni umma kumiliki mifumo ya uchumi (Africanization), baada ya kupata uhuru na kuhamasisha vijiji vya ujamaa.

“Alihakikisha Watanzania wanapata nafasi kwenye uongozi wa nchi...pamoja na kwamba hawakuwa na elimu na uzoefu kama Wazungu, lakini uzalendo na mapenzi yao kwa nchi yalimpa moyo kwamba watafanya vizuri,” anasema Wasira.

Akizungumzia namna alivyowawezesha wanawake, Wasira anataja kumruhusu mkewe Sophia kushiriki harakati za ukombozi hadi kufikia kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) ni jambo lisilosahaulika.

“Kwa sababu aliamini katika usawa wa watu wote, dini au mila na desturi havikuwa kikwazo. Na kwa hilo mkewe akawa mfano bora ambaye aliwajengea ujasiri wanawake wengi, waliokuwa wanadhani hawawezi wakaamini wanaweza na kushiriki harakati mbalimbali,” anafafanua.

Kwa upande wake, kada wa CHADEMA, Suzan Lyimo, anaanza kwa kueleza namna alivyowaamini wanawake kiasi cha kumruhusu mkewe Sophia kushiriki siasa.

Anasema Kawawa alimruhusu kipindi ambacho wanaume wengi walikuwa hawawaruhusu wake zao kufanya kazi hasa siasa na kwamba Sophia Kawawa alifanikiwa kujipambanua na kuleta mageuzi kwa kuwajengea ujasiri wanawake wengi.

“Mimi sio CCM wala UWT, lakini tunamkumbuka Kawawa kama kiongozi aliyeitumikia nchi kwa uaminifu. Mke wake aliwaunganisha wanawake... kwangu ukiacha Bibi Titi, mama Sophia ni mama shupavu na anadhihirisha kwamba penye mafanikio ya mwanaume, kuna mwanamke nyuma yake,” anasema Suzan.

Anaongeza : “Tunaona ni katika wale wamama wachache walioupenyeza katika ngazi za uongozi na mpaka leo tunajivunia kama wanawake na tunaendelea kuongezeka katika siasa.”

Anasema Kawawa atakumbukwa kwa mambo mengi kutokana na sifa zake za uongozi akiwa mnyenyekevu na mwaminifu kwa utumishi wa umma.

“Kawawa akiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za serikali, alisimamia utaifishaji wa mali kuhakikisha madaraka ya Waafrika yanabakia kwao. Pamoja na kwamba baadhi ya watu walilalamika, lakini ile kutufanya Waafrika tumiliki uchumi wetu aliisimamia vizuri... hapa ndipo jina la Simba wa Vita lilipoanzia,” anakumbusha akitaja operesheni vijiji vya ujama.

“Natokea Kilimanjaro, nakumbuka jinsi ambavyo ndugu zetu walihamishiwa Morogoro na sasa wanafurahia maisha huko. Leo tunajivunia uwepo wa vijiji hivyo japokuwa kuna watu walilalamika, leo wanafurahia matunda ya uamuzi huo,” anasema.

Anaeleza kuwa akiwa kwenye utumishi wa umma na safu yote iliyofanyakazi na Mwalimu Nyerere, Kawawa ni kioo cha uadilifu wasiojilimbikizia mali.

“Hivi sasa maadili yamepungua. Uongozi unatawaliwa na rushwa, enzi zile ahadi za mwanachama wa TANU ilikuwa rushwa ni adui wa haki, tofauti na sasa inaonekana ni rafiki... kwamba anayetoa hela nyingi ndiye anayepewa uongozi...na umekuwa ni wa kununua kuanzia udiwani, ubunge au ujumbe ndani ya chama,” anasema.

Anagusia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kusema kuwa inatoa picha ya namna baadhi ya watumishi na viongozi wa umma wasivyo waadilifu.

“Tunaona kwamba kila mwaka ripoti ya CAG kila mwaka inakuwa mbaya kuliko mwaka uliopita, unaona kwamba matatizo ya ubadhirifu hayadhibitiwi. Hii inatokana na watu waliopewa nafasi kukosa uzalendo na uadilifu. Inahitaji viongozi watakaokemea rushwa na wizi wa fedha za umma kwa vitendo,” anafafanua Suzan.

Kamishna mstaafu wa madini na mwana jiolojia, Dk. Peter Kafumu, anasema Kawawa alikuwa mnyenyekevu, mwaminifu, mtii

INAENDELEA UK. 14

KUELEKEA UCHAGUZI…

# Kinamama wachoka 'chenga za mwili' waibua Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake



Profesa Ruth Meena, mhadhiri mstaafu wa vyuo vikuu na mwanaharakati wa usawa wa kijinsia akizindua ilani ya Wanawake na Uchaguzi, kwenye Tamasha la Jinsia Dar es Salaam.

**Na Gaudensia Mngumi**

NI nyakati za uchaguzi, ulio kwenye ncha za vidole sasa ni ule wa serikali za mitaa, wakati wowote kuanzia sasa tarehe inatangazwa.

Oktoba mwakani ni uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani kwa Bara wakati Zanzibar ni rais wa SMZ, mwakilishi na diwani. Daftari la wapigakura, ilani na mchujo wa wagombea unapoanza ndani ya vyama kinamama wana jambo lao.

Ni Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake, ikiangazia uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2024 na mkuu wa 2025, yenye kauli mbiu Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi.

Ikizinduliwa mwaka jana kwenye Tamasha la Jinsia, linaloandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni mwendelezo wa madai ya wanawake wanaosisitiza umuhimu wa ushiriki wa kinamama katika uongozi wa nchi na siasa.

Ilani inatamka kuwa wanawake ni wadau na washiriki wakuu katika michakato mbalimbali ya uchaguzi wana nafasi na umuhimu mkuu wa kuwa sehemu ya uongozi wa kisiasa na wa taifa.

Wanawake ni wengi zaidi ya asilimia 51 ya watu milioni 61 wa taifa hili,takwimu za sensa ya mwaka 2022 zinasema, lakini kwa upande mwingine wana nguvu ndogo kiuchumi na kisiasa jambo ambalo linadhoofisha mchango wao katika maendeleo ya taifa.

Ni kama kuacha idadi kubwa ya Watanzania nje ya uongozi na maamuzi yanayowahusu wao wenyewe. Iwapo idadi yao ni zaidi ya milioni 33.13 ni wazi kuwa ndiyo wengi kwa kila idara kuanzia kupigakura, uzalishaji mashambani, wajasiriamali na watumia huduma muhimu kuanzia za tiba hadi nishati.

Lakini cha kushangaza idadi yao si kubwa kwenye ushiriki wa masuala ya kisiasa na uongozi wa umma, kwenye elimu na wale wenye nguvu kubwa kiuchumi. Ndiyo maana muda wote wana madai ya kutaka kuona mwanamke anashiriki siasa na anaongoza jamii na taifa lake.

Ilani ya Wanawake 2023, inabainisha kuwa kwa miaka mingi hapajakuwepo na utashi wa kisiasa wa kubomoa misingi inayokwamisha wanawake kwenye kushiriki kama raia huru katika chaguzi zote zilizopita.

"Walengwa wa kwanza ni sisi wanawake ambao ni wapigakura wenye nia ya kushiriki katika uchaguzi na hatimaye kuwa sehemu ya uongozi wa taifa letu kwenye maeneo mbalimbali.

"Ilani hii ni wito kwetu wanawake wote kuungana na kupaza sauti tukiwa na ajenda moja ya kudai mabadiliko ya mfumo au mifumo kandamizi na yenye kutubagua. Wanawake tunasema hatuwezi kujenga demokrasia thabiti kama chaguzi si huru na haki kwa mtazamo wa kijinsia," inasema sehemu ya andiko hilo.

Wanawake wanailenga serikali na kuitaka ihakikishe taasisi na vyombo vyote vinavyohusika na uchaguzi vinawajibika kuzingatia mikataba, itifaki, matamko ya kimataifa na kikanda pamoja na misingi ya kikatiba iliyoainishwa kwenye dira ya taifa ya 2025.

"Kwetu sisi wanamtandao wa wanawake na katiba, uchaguzi na uongozi, masuala tuliyoibua katika ilani zilizopita pamoja na yale tuliyobainisha wakati wa mchakato wa kutayarisha katiba mpya na kuingizwa kwenye katiba iliyopendekezwa ya Oktoba 2014 , bado tunaona mafanikio madogo sana.

Ni kiasi kidogo kwenye ngazi nyingi za uongozi na kwamba mfumo dume unazidi kujiimairisha katika nyanya mbalimbvali na kwa kutumia mikakati mbalimbali pia," inaeleza Ilani ya Wanawake 2023.

Ilani ya 2023 ni ya sita ikitanguliwa na nyingine tano zilizoandaliwa wakati wa mwaka wa uchaguzi mkuu kuanzia 2000 hadi 2020.

Itakumbukwa kuwa ilani hiyo ina sauti za wanamtandao wanawake, katiba, uchaguzi na uongozi, wenye takribani asasi za kiraia 175 kuanzia ngazi za chini kwenye jamii hadi taifani.

Aidha, inaitaka serikali kuchukua hatua za makusudi kuondoa vikwazo vinavyoendeleza ubaguzi katika ushiriki wa wanawake katika uchaguzi kama wagombea wa nafasi mbalimbali na wapigakura na kusawazisha uwanja wa demokrasia.

Usawa unaotajwa kwenye ilani hiyo ni pamoja na matumizi ya rasilimali za uchaguzi kuwanufaisha wagombea wanawake na wanaume na kusimamia mchakato wote ili uwe huru na haki kwa mrengo wa kijinsia.

Kuhusu vyama vya siasa ilani inavitaka vione faida ya kufungua milango kwa wanawake ili kujenga demokrasia thabiti ndani ya taasisi hizo. Hii ni kwasababu vina uwezo mkubwa wa kuamua ni nani anayeingie kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, nani afungiwe milango na ni nani aungwe mkono hadi hatua za ushindi.

Halikadhalika inavihamasisha vyama kufungua milango kwa wanawake ili kujenga demokrasia thabiti ndani ya vyama , lakini pia kuonyesha nguvu ya kura zao kwenye uamuzi wa mwisho kwa nani waatkayempa dhamana ya kuongoza taifa kwa kipindi cha miaka mitano mingine.

Vile vile ilani inalenga wapigakura wote hasa wanawake kukataa takrima au kununuliwa ama kudanganywa kuuza kura zao kwa wenye uchu wa madaraka ambao hawana nia ya kuwasilisha sauti zao.

Ilani inalenga serikali itakayochaguliwa iwajibike kutekeleza na kuchukua hatua stahiki ili kufanikisha dira ya taifa ya kuondoa ubaguzi wa aina yoyote ikiwa ni pamoja kutokomeza ubaguzi wa kijinsia.

Aidha, inataka kuwepo mabadiliko ya kutokomeza mfumo kandamizi inayohalalisha ubaguzi wa wanawake katika uchaguzi kama wapigakura wenye kuwania nafasi za uteuzi na hatimaye kuwakwamisha kwenye kuchaguliwa kama wawakilisha wa wanchi katika ngazi mbalimbali.

Inataka ziwepo fursa wezeshi na utashi wa kisiasa ndani ya jamii , vyama na uongozi wan chi wa kuleta mabadiliko makubwa kwenye mifumo yote kandamizi ikiwa ni pamoja na ule wa uchaguzi na kwamatinki hiyo.

**UKATILI VS WANAWAKE**

Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni tatizo kubwa na unatumika kama njia ya kudhibiti na kukandamiza kinamama na watoto wa kike.

Licha ya kuwepo kwa jitihada mbalimbali za kuutokomeza , takwimu zinaonyesha kuendelea kwa tatizo hilo ambalo ni tishio kwa ustawi wa wanawake ambao ni sehemu kubwa ya raia wa nchi hii.

Mpango wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi wanawake na watoto Tanzania kuanzia 2017 hadi 2022 unabainisha kwamba wanawake katika ngozi zote hupitia aina nyingi za ukatili kama wa kisaikolojia, kuumizwa kimwili, ukatili na kingono unaohusisha rushwa ya ngono.

**MADAI MUHIMU**

Ilani inaikumbusha serikali kutumia idara na taasisi zake kusawazisha uwanja wa ushindani na kuweka taratibu za kufikia lengo la usawa wa kiuwiano wa 50/50 kwenye uongozi wa taifa.

"… tukiwa wapigakura tunasema kwa sauti moja kwamba wajibu wa srikali iliyoko madarakani ni kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili wanawake washiriki kikamilifu kwenye uchaguzi bila vipingamizi vinavyotokana na mifumo ya kibaguzi ndani ya nchi."

Wanawake wanataka kuboresha sheria za uchaguzi kwa kuondoa mapengo na vikwazo vinavyobagua wanawake.

Aidha, Wizara ya Sheria na Katiba inahimizwa kurekebisha sheria zenye viashiria vya kuhalalisha mianya ya ubaguzi dhidi ya wanawake kwenye uchaguzi.

Baadhi ya sheria hizo ni ile ya uchaguzi isiyoweka mkazo katika teuzi za wanawake wagombea kwenye vyama vya siasa.

Nyingine ni sheria ya gharama za uchaguzi inayowabebesha wagombea mzigo wa gharama bila kujali tofauti za kiuchumi kati ya wanawake na wanaume.

# Maandamano ya CHADEMA ndivyo, R4 zinavyoibeba demokrasia



Mamia ya wafuasi wa CHADEMA wakishiriki mandamano ya amani jijini Dar es Salaam. **PICHA :HALFANI CHUSI.**

**Na Halfani Chusi**

DEMOKRASIA imekua, falsafa ya R4 za Rais Samia Suluhu Hassan, zikianza kuonekana kwa vitendo, R4 ni maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya taifa letu.

Mageuzi ya kidemokrasia kwa sasa ni makubwa, uhuru wa watu kuongea na kutoa maoni nao ni mkubwa, hata vyombo vya habari pia viko huru.

Nyota njema na mfano wa haya yote, ni hatua yake serikali iliporuhusu CHADEMA, kuandamana kwa amani bila kubughudhiwa huku Jeshi la Polisi likisimamia ulinzi kama sheria na katiba inavyoeleza.

Maandamano yao yaliyodumu kwa saa 11 yalitawaliwa na ujumbe unaohitaji serikali kuwajibika kwa wananchi. Mojawapo ni zile zinasomeka:

"Tunataka katiba mpya, tunataka bei ya sukari ishuke, maboresho sheria za uchaguzi, maisha magumu, serikali isikilize hoja za wananchi, waliotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG kuhusu ubadhirifu wa mali za umma wachukuliwe hatua." Ni baadhi ya mabango yalivyosomeka waliyokuwa wamebeba waandamanaji hao.

Hata hivyo, katika maandamano yao pamoja na kuwapo kwa ratiba kwamba yangeanza saa 3:00 asubuhi, wapo waliofika Stendi ya Maramba Mawili Mbezi jijini Dar es Salaam, saa 11 alfajiri.

Inapofika majira ya saa 2:00 asubuhi mamia ya watu yalianza kumiminika katika viwanja hivyo ambavyo viliandaliwa kwa ajili ya kukutana kuanza kuandamana.

Inapotimu majira ya saa 4:00 asubuhi, msafara unaondoka Maramba kuelekea makao makuu ya Umoja wa Mataifa (UN), yaliyoko Barabara ya Sam Nujoma karibu na Mlimani City, huku wafuasi wakiunga safari hiyo kwa miguu kutoka Mbezi mhadi ofisini hapo.

Wakati msafara huo ulipoziba barabara nzima na kusababisha foleni, ukipambwa na kukolezwa moto kwa nyimbo za chama chao, pembeni ya mitaa ya barabara ya Morogoro ulikokuwa unapita msafara umati wa watu ulifurika kuangalia maandamano hayo huku baadhi yao wakiunga mkono kwa kunyoosha vidole viwili juu kama ishara ya kuitaja CHADEMA.

Kuanzia vikongwe hadi watoto nao waliitikia wito, walipofika Kibanda cha Mkaa, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, aliungana na waandamanaji hao akitokea uwanja wa ndege.

Anapoonekana ghafla shangwe zinaibuka kutoka kwa wafuasi hao na ikiwa jambo lililoongeza furaha na hamasa zaidi.

Inamlazimu Lissu na viongozi wengine kutembea kwa miguu hadi Ubungo, ndipo akapanda gari akionekana kwa juu huko akisalimiana na wafuasi wa chama hicho waliokuwa wamefurika pembezoni ya barabara.

Polisi pia walikuwa bega kwa bega katika msafara huo wakiwalinda, wengine walionekana wakisistiza amani katika hali isiyo ya kawaida moja wa kada wa CHADEMA akiwagawia maji ya kunywa huku akisema wamechoka na jua wanapaswa kunywa maji, mwingine alikuwa ameshika bango liliandikwa kikotoo kwa polisi kiondolewe huku akilisogeza machoni mwa polisi.

Msafara huo ulipofika UN, watu waliokuwa karibu na maeneo hayo walisogea eneo hilo na walipokelewa na Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo huku akiwahakikishia amani.

Lisu, Mbowe na viongozi wengine wawili kutoka kwenye chama hicho waliruhusiwa kuingia ndani na kundi jingine lilikuwa limeongozana na msafara huo lilizuiliwa mpaka pale walipotoka na kuongea na umma.

Nje ya ofisi hizo, wafuasi hao wananyoosha mabango juu yenye ujumbe kuanzia "tunataka katiba mpya, tunataka uchaguzi wa uhuru na haki, maboresho sheria za uchaguzi hadi tume huru ya uchaguzi."

**MTAZAMO WADAU**

Akizungumza katika maandamano hayo Wakili wa Kujitegemea na Mwanaharakati wa Kutetea Haki za Binadamu, Boniface Mwabukusi anasema hiyo ni ishara ya taa ya njano kwa serikali.

Anafafanua kuwa maandamano yamefanyika kwa sababu serikali haisikii kero na maoni ya wananchi akisisitiza kuwa tukio hilo ni ishara ya kuionyesha nini wananchi wanataka.

"Sio vita, ukiona watu wanaandamana kwa sababu kuna mtu hasikii, hii ni hatua ya kumuonyesha mtawala, sio ghasia ni kuongea lugha ngumu kwa njia ya amani.

"Kama hatua hii isipoleta matokeo tutaanza kuandamna hata kwa kugoma kununua bidhaa zao, tutagoma hata kwenda kazini, ilimradi hatuvurugi amani yao, kuna taa ya kijani, njano na nyekundu kwa leo ni taa ya njano" anaongeza Mwabukusi

Aidha, wanafikisha ujumbe kwa serikali iwasikilize chama pinzani akidai taifa ni la wote, na kwamba kuna ulazima wa kufuata sheria ili anapoingia mtawala au mpinzani ifuatwe, anaongeza.

"Tumeona vikokotoo, wao hawalipi kodi, wananchi wanyonge ndiyo wanakandamizwa watu wa chache ndio wanaendesha nchi hii , wakati wachache wanakula na kuneemeka kwa hiyo nchi hii inahitaji bunge bora na linapatikana kwa katiba mpya" anasema Mwabukusi.

Wakili huyu anayepata umaarufu mkubwa baada ya kufungua kesi kupinga mkataba wa bandari, anakuwa ni kivutio cha aina yake.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), nacho hakiko nyuma kuhusiana na hatua hiyo ya kuandamna kupitia Mkurugenzi wake Mtendaji Anna Henga, anasema kitendo cha serikali kuruhusu chama hicho kuandamana kwa amani, ikiwa ni jambo la kikatiba anaona hiyo ni dalili njema huku akisisitiza kwamba kufanya hivyo ni haki yao kisheria.

Dk Anna, ambaye pia kitaaluma ni mwanasheria anasema: "kuandamana ni haki ya kujieleza, hata ukienda mahakamani ukishindwa kesi lakini kama ulipewa haki ya kujieleza inasaidia kuliko kunyimwa, vile wanavyodai vingine ni vigumu kidogo laiki ni vingine inawezekana.

"Dai lao la kushusha miswaada linawezekana kwa hiyo vipo vinavyowezekana na visivyowezekana lakini cha muhimu wamepewa haki yao ya kujieleza jambo ambalo lilikuwa halifanyiki utawala uliopita" anasema Dk Anna

Pia anakosoa kauli ya Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam Jumanne Muliro, akisema zamani walikuwa wanazuia kuandamana kutokana na kauli za viongoZi wa vyama pinzani za vitisho ikiwamo kusema 'tutaandamana na damu lazima imwagike.'

"Sio kweli bwana, hivi mtu anaandamana amebeba karatasi mkononi anamwagaje damu? Amebeba kabango anafikisha ujumbe anamwagaje damu? Kwahiyo lazima atafute natoka vipi kwa sababu anaweza akaulizwa kwa nini mlikuwa hamruhusu zamani?

"Anaweza akatoka mtu mmoja kwenye mtandao, akasema maneno ya kutisha lakini wewe kama kiongozi imara ni taasisi kama Jeshi la Polisi, huwezi kumuogopa mtu wa aina hiyo." anasema

"Kwa sababu wana silaha na wamefundishwa walishindwaje kuwadhibiti watu kama hao? Mpaka sheria ya makosa ya kimtandaoa imetungwa unashindwaje, unanyima haki za watu wengi kwasababu mtu mmoja aliyesema hivyo," anahoji Dk Anna

**MAKADA CHADEMA**

Wakizungumza na waandishi wa habari, baadhi ya makada wa CHADEMA, wanaeleza kufurahishwa na namna polisi walivyolinda maandamano hayo.

Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, anasema polisi wameshirikiana vizuri na raia kiasi cha kupeana maji ya kunywa.

"Sijaona polisi mwenye silaha, wameshirikiana na wananchi kwa namna ya ajabu. Hakuna aliyepoteza kitu wala aliyejeruhiwa hii maana yake ni kwamba wananchi wanataka mabadiliko bila fujo," anashudia.

Mwanaharakati Ananilea Nkya, anasema ameungana na wafuasi wa CHADEMA kuwakilisha kundi la watu wasio na vyama kudai katiba mpya, tume huru ya uchaguzi na kushinikiza miswada mitatu ya masuala ya uchaguzi iondolewe bungeni.

"Miswada hii kama itapitishwa na kuwa sheria haitaleta mabadiliko yoyote chanya kwa sababu wakurugenzi wa halmashauri wamekuwa wakivuruga chaguzi kwa kuwa ni makada wa CCM," alisema.

Akiwaaga wananchi na wafuasi wa CHADEMA saa 10:17 jioni makao makuu ya UN karibu na Mlimani City , Mbowe anasema wataitisha maandamano katika mikoa mingine.

"Nawashukuru wanachama wetu waliosafiri kutoka mikoa mbalimbali kuja kutuunga mkono, nawashukuru wote mliojitokeza leo, naishukuru ofisi ya UN kwa kutupokea na ninalishukuru jeshi la polisi kwa ushirikiano waliotupatia," alisema.

**NENO LA POLISI**

Katika maandamnao hayo Kamanda Muliro, anawataka wanasiasa kuchunga ndimi zao. "Yaliyokuwa yakileta msuguano kati ya wasimamizi wa sheria ni aina ya kauli za awali zilizokuwa zikitolewa na baadhi ya viongozi wa vyama, haiwezekani polisi akakaa kimya asijiandae kwa mtu kutangaza wiki kabla kwamba damu itamwagika.

"Itakuwa polisi mjinga mtu anasisitiza kauli hiyo halafu unakwenda unamuangalia kama vile ni mwanachama wa SACCOS ya Kitunda. Polisi hawezi kukuruhusu utembee hata hatua mbili.

"Haya ni mabadiliko makubwa hata kwa wao (CHADEMA) walikuwa wakisisitiza amani, tena mara kadhaa. Tumewaita tumepima akili na kauli zao na wanavyotamka. Nafikiri ni hatua nzuri na muhimu, warekebishe kauli zao turekebishe vitendo vyetu," alisema.

UCHAGUZI MAREKANI

# 'Mambo yanapogeuka, msiyempenda anakuja'

Na Mwandishi Wetu

KIONGOZI wa zamani wa Marekani, Donald Trump, anaelekea kuwa mgombea wa Republican atakayechuana na Rais wa sasa Joe Biden, ukiwa ni ujumbe kuwa hata kama wapo waliowaza vinginevyo dhidi yake, anaweza kurejea ikulu kwa kasi.

Chama cha Republican kinaelekea kumteua kuwa mgombea wake 2024, baada ya kuwabwaga wapinzani wake wote huko jimboni Iowa karibuni.

Ushindi unaompa kura nyingi kuliko wagombea wote kwa pamoja na huenda akarejea tena ikulu baada ya uchaguzi wa Novemba 5, 2024, inasema BBC.

Kwa upande mwingine, mtandao wa Aljazera, unasema Waamerika wana jambo lao nalo ni kutaka nchi yao irudishwe kwenye heshima yake.

Ndicho wanachotamani sasa, wanaona Donald Trump akiingia tena kwenye mioyo yao tangu kuanza mwaka huu.

Kuanzia mgogoro wa Gaza ambako Amerika ya Joseph Biden haijafanya kitu hadi kuyumba kwa uchumi, wapigakura wengi wa Serikali ya Wananchi au GOP wanapendelea kurejea kwa Trump madarakani, msimu wa uchaguzi wa urais unapoanza.

Mambo ni moto, kuanzia Iowa, vyombo vya habari vinasema nchi ilikuwa imeganda theluji baridi ikiwa chini ya sifuri 'O' lakini "baridi ya hatari", kwa mujibu wa maofisa wa eneo hilo, haukuwazuia kusema ndiyo kwa Trump.

Hata theluji na hali ya hewa ya baridi kali haikuzuia mamia ya watu kutoka nje kumwona Rais wa zamani Donald Trump huko Indianola mji mdogo kusini mwa mji mkuu wa jimbo wa Des Moines, ukiwa na shangwe kubwa zaidi.

Huko jimboni Iowa kulikofanyika mikutano na mijadala wafuasi wa Trump, walivaa kofia na shati zenye ujumbe wa 'Make America Great Again (MAGA) zilizo na picha ya rais wa zamani na wakimaanisha kushikilia misimamo yake na kumuunga mkono mwaka 2024 kwenye mkutano wa kampeni.



Donald Trump akizungumza kwenye mji wa Des Moines, Iowa, Januari 15 , 2024:**PICHA: BLOOMBERG**

Itakumbukwa zaidi ya miaka mitatu baada ya wafuasi wake kuvamia Ikulu ya Marekani kuzuia kuidhinisha ushindi wa Rais sasa, Joe Biden na mashtaka manne ya jinai baadaye kufunguliwa dhidi yake , uungwaji mkono wa Trump miongoni mwa Wana Republican ni dhahiri.

George Hutton, mfuasi kindakindaki wa Trump kutoka kaunti jirani ya Madison ambaye alihudhuria mkutano huo wa Iowa, anasema wapinzani wa rais huyo wa zamani wa chama cha Republican - Gavana wa Florida Ron DeSantis na mjumbe wa zamani wa Umoja wa Mataifa Nikki Haley - "wanapoteza wakati wao".

"Nadhani Trump atashinda kwa zaidi ya kile wanachokikisia," Hutton anasema, akimaanisha ushindi wa Iowa.

### KILIO UCHUMI

'Tunataka nchi yetu irudi kileleni' ndicho wapigakura wa Trump wanachotaka. Wakati kwa Wamarekani wengi, miaka ya Trump ilikuwa na machafuko, matamshi ya uchochezi na kuongezeka kwa ubaguzi hasa kuchukia Weusi, wafuasi wa rais huyo wa zamani wanatamani tena hali ile wakati alipokuwa Ikulu wakisema Oval Office.

Baadhi ya wafuasi wa Trump wanaohojiwa na vyombo vya habari wanataja sababu tatu kuu kwa nini wanamuunga mkono rais huyo wa zamani.

Mosi uchumi kudorora, rekodi ya viwango vya wahamiaji wanaofika kwenye mpaka wa kusini kuongezeka na ukosefu wa utulivu wa duniani hasa Ukanda wa Gaza. Kadhalika Trump anaposongwa na matatizo yake ya kisheria pia vinamwongezea huruma kutoka kwa wapigakura.

### TRUMP MAHAKAMANI

Donald Trump anakabiliwa na mashtaka manne ya uhalifu, hali ambayo haijawahi kutokea kwa rais wa zamani wa nchi hiyo. Hata hivyo, kesi hizo zimemwongezea umaarufu kati ya wanachama wa Republican.

Tayari amejizolea asilimia 49 za uungwaji mkono katika chama chake, kwa mujibu wa utafiti wa maoni na anakaribia kuteuliwa kupambana na Biden, inasema DW na anapata nguvu zaidi baada ya kushinda mchujo wa kwanza katika jimbo la Iowa, ambapo alijizolea zaidi ya nusu ya kura zote.

Kwa mujibu wa DW, washirika wa Rais Joseph au Joe Biden, wanaamini kuwa yeye ndiye mgombea pekee wa Demokrat anayeweza kumshinda Trump. Utafiti wa maoni wa hivi karibuni zaidi wa shirika la Reuters/Ipsos ulimpa asilimia 35, kiwango sawa na jinsi Trump anavyoungwa mkono.

Kwa mara nyingine Kamala Harris atakuwa mgombea mwenza suala la uchumi litachangia pakubwa katika kampeni yake ya kutaka kuchaguliwa tena.

Japo Marekani iliepuka mdororo wa uchumi uliotarajiwa na inakua kwa kasi zaidi kuliko wachumi walivyotarajia, mnamo mwaka 2022, mfumuko wa bei ulifikia kiwango cha juu zaidi kuwahi shuhudiwa kwa miaka 40 iliyopita na gharama ya chakula na gesi inawaelemea wapigakura.

Biden ameongoza mwitikio wa serikali za nchi za Magharibi kwa uvamizi wa Urusi nchini Ukraine na kuwashawishi washirika kuiwekea vikwazo Moscow na kuunga mkono Kyiv na amekuwa akiunga mkono Israel katika mzozo wake na wapiganaji wa Hamas huko Gaza.

Hata hivyo, amekabiliwa na ukosoaji mkali kutoka kwa baadhi ya watu ndani ya chama chake kwa kushindwa kuunga mkono wito wa kusitisha mapigano eneo la Palestina, ambapo maofisa wa afya wa Gaza wanasema zaidi ya watu 25,000 wameua, DW inasema.

## MZALENDO, MWANAMAPINDUZI HALISI AMBAYE HATA SASA KAZI ZAKE ZINAISHI

INATOKA UK. 11

fu, asiye na makuu, wala tama ya mali, mpatanishi na aliyependa kuwatumikia watu.

"Viongozi wa sasa wanapaswa kuiga kwake. Uadilifu wake usiotiliwa shaka ulifanikisha mipango mingi ya kuiwezesha nchi kupata maendeleo. Asingekuwa mtii ni wazi nchi ingeingia kwenye mgawanyiko mapema sana, lakini alishirikiana na Mwalimu Nyerere kujenga nchi baada ya uhuru na ndio maana alishika nyadhifa za juu serikalini kama msaidizi wa karibu wa baba wa taifa," anasema Dk. Kafumu.

Anaongeza kuwa: "Hivi sasa tumekuwa na viongozi machawa ili aendelee kuwepo kwenye nafasi. Kawawa hakuwa chawa. Moyo wake na matendo yake yalifanana. Leo hii unaona maneno na matendo ya baadhi ya viongozi wetu haviendani."

### HISTORIA YA KAWAWA

Alizaliwa Mei 27, 1926 Kijiji cha Matembwe, wilayani Songea, mkoa wa Ruvuma na kufariki Desemba 31, 2009. Ameshika nyadhifa mbalimbali serikalini na ndani ya TANU.

Alikuwa Waziri Mkuu kwa miaka 15 kuanzia Januari, 1962 hadi Februari 1977, alipomwachia kijiti Edward Sokoine.

Aliwahi pia kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania. Mbali ya nyadhifa hizo kubwa, sifa zake zilivuma alipokuwa kiongozi wa jumuiya ya wafanyakazi aliyetoa msukumo mkubwa kwa TANU kwa kulifanya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanganyika kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na chama hicho.

Historia inaonesha kwamba mwaka 1955 Kawawa alikutana na Mwalimu Nyerere na kumkabidhi Sh. 500 ambao ulikuwa mchango wa Chama cha Tanganyika cha Watumishi Waafrika Serikalini, chama ambacho Kawawa kwa wakati huo alikuwa Rais wake. Mchango huo ulikuwa ni kwa ajili ya nauli ya Mwalimu Nyerere kwenda Marekani kuhutubia Baraza la Umoja wa Mataifa (UNO).

Mbali na majukumu hayo, Kawawa alikuwa Mbunge wa Nachingwea mkoani Lindi na baadaye Liwale kuanzia mwaka 1965 hadi 1985. Ndani ya TANU na CCM, amekuwa mjumbe na Katibu Mkuu wa CCM mwaka 1980 na Makamu Mwenyekiti wa CCM mwaka 1982 na mjumbe wa kudumu wa Halmashauri Kuu ya CCM.

Utumishi uliotukuka ulimpa tuzo mwaka 2007 baada ya Chuo Kikuu cha Massachusetts Dartmouth kumtambua kama mpiganaji mkubwa wa uhuru, usawa na haki barani Afrika. Alitunukiwa tuzo ya Drum Major Award, tuzo ya kumbukumbu ya urithi wa Dk. Martin Luther King Jr, Mmarekani mweusi mpigania usawa na haki za Waamerika.



# Watumishi 400 kupatiwa mafunzo ya teknolojia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeanza maandalizi ya ujenzi wa Chuo Mahiri cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) jijini hapa na kutangaza ufadhili kwa watumishi 440 wa umma wa mafunzo ya teknolojia zinazoibukia ili kuwaongezea ujuzi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohammed Khamis Abdulla, alisema chuo hicho kitakachojengwa eneo la Nala kitakuwa pia kinatoa mafunzo kwa vijana na wabunifu nchini ya usalama wa mifumo ya mawasiliano na utengenezaji wa mifumo ya teknolojia hiyo.

"Chuo hiki kitakuwa ni tofauti na vyuo vingine ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo ya ujuzi kwa muda mfupi kwa njia ya moduli kulingana na mahitaji kwa nyakati husika."

"Baada ya moduli kuisha mhitimu atakuwa amepewa ujuzi kwenye eneo mahsusi na kumuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija, na hii itapelekea vijana wengi kujiajiri kwa haraka au kuajiriwa Sekta ya TEHAMA kulingana na mahitaji," alisema.

Alisema kuanzishwa kwa chuo hicho nchini kutasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana nchini.

"Kuna vijana wenye vipaji ambao hawajasoma shule, kupitia chuo hiki wengi watapatiwa ujuzi na kuweza kuendana na mapinduzi ya 4,5 na 6 ya viwanda. Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chuo katika hatua za awali unagharamiwa na serikali kwa kuwezesha upembuzi yakinifu na uandaaji wa mitaala na miongozo ya chuo hicho," alisema.

Alisema fedha za ujenzi wa chuo hicho ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia Benki ya Exim ya Korea.

Kwa mujibu wa Abdulla, Shilingi Bilioni 80 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho mkoani Kigoma, unaotarajiwa kuanza mapema mwaka huu.

"Vyuo hivi vitaifanya Tanzania kuwa mahali pazuri pakuvutia utalii wa kidigitali kujifunza na kuongeza uwekezaji kutokana na upatikanaji endelevu wa jamii yenye maarifa kuendana na kasi ya mabadiliko," alisema.

Kuhusu mafunzo, alisema Serikali imeweka mpango wa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa umma 500 kwenye kozi za kuongeza ujuzi kuhusu TEHAMA hususani teknolojia hizo zinazoibukia.

Alisema kwa awamu ya kwanza, watumishi 20 wamefadhiliwa katika mafunzo ya muda mrefu vyuo vikuu nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza ujuzi.

"Tupo kwenye maandalizi ya mwisho ya kupeleka wataalamu 40 kwenye mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi, kati ya hao 15 maprofesa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dodoma na Mbeya ya teknolojia zinazoibukia na watakapomaliza wataendelea kutoa mafunzo katika vyuo walivyotoka na wakati Chuo Mahiri cha TEHAMA kinaendelea kujengwa," alisema.

Alisema nafasi 15 watatoa kwa watumishi wa Benki Kuu , Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhusu matumizi ya akili bandia na nafasi 10 kwa watumishi mafunzo ya anga za juu.

"Napenda kuwatangazia watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa tumefungua dirisha la maombi hayo kupitia tovuti ya www.scholarship.go.tz," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu, alishukuru uamuzi wa serikali kujenga chuo hicho Dodoma na kuahidi kutoa ushirikiano ili kufanikisha.



Diwani wa Kata ya Kizota, jijini Dodoma, Jamal Ngalya, akizungumza na wafanyabiashara wa umoja wa wauza utumbo wa soko la Mbuyuni juzi, kuhusu kuruhusiwa kufanya biashara baada ya katazo la kuwazuia kwenye eneo hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vita dhidi ya ukoma yaja nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MRATIBU wa Kudhibiti wa Ukoma nchini, Dk. Deus Kamara, amesema serikali imeweka mikakati ya kutokomeza ugonjwa huo nchini kwa kuwafuata wagonjwa katika jamii badala ya kuwasubiri vituo vya afya na hospitali.

Dk. Kamara alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini na jitihada zinazofanywa na serikali kuudhibiti.

"Mikakati ambayo tumeiweka na tunataka wadau na serikali kuwekeza kwenye eneo hilo ni pamoja na kuongeza hamasa kwa jamii kuhusu Ukoma, kufuata wagonjwa kwenye maeneo yao badala ya kuwasubiri waje hospitalini, pia kuwekeza kwenye tiba kinga," alisema.

Alisema kwa kutoa hamasa, jamii itafahamu ugonjwa huo na dalili zake ili wagonjwa wafikishwe hospitalini mapema kupata tiba na kudhibiti kuambukizwa wengine.

"Kwa kuwafuata wagonjwa katika maeneo yao kutasaidia kuwabaini mapema na kupata tiba tofauti na ilivyo sasa ambavyo wamekuwa wakichelewa na kupata madhara zaidi," alisema.

Alisema pamoja na Tanzania kupiga hatua kudhibiti ugonjwa huo kuna mikoa 10 nchini inaripotiwa kuwa na wagonjwa 50 hadi 200 kwa mwaka.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Morogoro, Lindi, Tanga, Katavi, Dar es Saalam, Geita, Tabora, Dodoma, Mtwara na Ruvuma. Dk. Issa Galimo kutoka Shirika la Ujerumani linalojihusisha na mapambani dhidi ya Ukoma na Kifua Kikuu ( GLRA), alisema takwimu zinaonyesha mwaka 2022 Tanzania ilikuwa na visa vipya na vilivyojirudia vya ugonjwa huo wa ukoma 1,837.

Dk. Galimo, alisema kama shirika wamekuwa wakishirikiana na serikali kwenye mapambano dhidi ya ukoma kwa hafua mbalimbali.

"Kama mnavyofahamu Serikali haiwezi kufanya kila kitu yenyewe, hivyo sisi tumekuwa tunafanya shughuli mbalimbali kwenye mapambano haya ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huu," alisema

Alisema kutokana na ugonjwa huo kuambaukiza kwa njia ya hewa, wamekuwa wakitoa elimu kwa umma kuepuka misongamano na nyumba kujengwa kwa kuwekwa madirisha makubwa yanayopitisha hewa.

"Pia tunatoa elimu kuhusu jamii kuachana na tabia ya kuuhusisha ukoma na imani za kishirikina ama kuwa ni wa kurithi jambo ambalo siyo kweli," alisema.

Hata hivyo, alisema moja kati ya dalili za mgonjwa wa Ukoma ni kuwa na matabaka ambayo hayawashi wala hayana hisia katika ngozi na mishipa ya fahamu kuvimba.

"Kwa mtu ambaye ana matabaka matano huo ni ukoma hafifu na mwenye mabaka zaidi ya matano katika mwili wake huo ni ukoma mkali," alisema.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), ukoma umepungua nchini na kuna mikoa nchini ambayo kwa kipindi cha takribani miaka mitano hauna kisa ambacho kimeripotiwa.

## 'JKT acheni kupikia kuni, mkaa'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Stergomena Tax amelitaka jeshi hilo kutumia nishati safi na kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa ili kutunza mazingira nchini.

Dk. Tax alitoa wito huo jana wakati akipanda miti katika makao makuu ya jeshi hilo yaliyopo wilayani Chamwino Mkoa wa Dodoma ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano nchini.

Alisema kuanza kwa matumizi ya nishati safi, kutasaidia kudhibiti uchafuzi wa mazingira na ukataji miti ovyo katika maeneo mbalimbali nchini.

Alilipongeza jeshi hilo kwa kupanda idadi kubwa ya miti nchini huku akisisitiza itunzwe ili iweze kukua vizuri.

Waziri huyo alilitaka jeshi hilo kuendelea kupanda miti ili kuikifanya Dodoma kuwa ya kijani na maeneo mengine kama serikali inavyoelekeza katika kampeni yake ya kitaifa.

Alisema JKT imekuwa ikiyaenzi kwa vitendo maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwa na Tanzania ya Kijani katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kupanda na kutunza miti.

"Nawaelekeza JKT kufanya thathmini ya miti yote iliyokwisha pandwa, mingapi imekua na JKT wataendelea kuhakikisha wanatekeleza yale ambayo Rais, anatarajia kuyaona ili kuhakikisha wanakuwa na Tanzania ya Kijani," alisisitiza.

Mkuu wa Tawi la Utawala, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema wameanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philipo Mpango la kutunza mazingira kwa kutumia nishati mbadala na kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa katika vikosi vyote vya jeshi hilo.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Hamza Hamis Chilwa, alilipongeza jeshi hilo kwa kutekeleza agizo la Dk.Mpango la kuzitaka taasisi zote zinazolisha watu zaidi ya 10,000 kutumia nishati mbadala.

Chilwa alisema wameanza matumizi hayo katika vikosi vyao vyote na kwa mba kwa kupanda miti na kuanza matumizi ya nishati mbadala ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inayoelekeza kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

Naibu waziri huyo, alisema jamii ya Watanzania inataaluma ndogo katika utunzaji wa mazingira, wengi wanaamini kukataa mti na kutengeneza mkaa ni haki yao ya msingi.

"Changamoto iliyopo ni miti iliyopandwa haitunzwi wala kushughulikiwa, hapa nitoe maelekezo kila mtu aliyepanda mti ashughulikie na kutunza, tulitoa maelekezo kila ifikapo Maadhimisho ya Siku ya Kuzaliwa Rais Samia, Januari 27 kila wizara ihakikishe inapanda miti 60,"alisema.

Chilwa alisisitiza kuwa katika kuelekea maadhimisho hayo, Watanzania waendelee kuhakikisha wanalinda Muungano kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo upandaji miti.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mkakati wa mkoa ni kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri ifikapo msimu wa mvua na kulipongeza jeshi hilo kwa kutunza kikamilifu eneo la Mzakwe ambalo ni chanzo kikuu cha maji.





# Matokeo ya sensa kuwadhibiti 'wanaoghushi' taarifa za mali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MATOKEO ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yametajwa kuwa ni mwarobaini wa kuwadhibiti wananchi kutoa taarifa za uongo kuhusu mali zao wakati wa kufanya tathmini ya athari za majanga ya asili yanapotokea na kusababisha uharibifu na upotevu wa mali.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Anne Makinda, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa mafunzo ya matumizi ya matokeo ya sensa ya mwaka 2022 kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe yaliyoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Alisema wakati wa maandilizi ya sensa hiyo, zilipigwa picha za satelaiti kwenye kila eneo nchini kwa ajili ya kuonyesha makazi ya watu, mifugo na mali nyingine zilizo kwenye maeneo hayo na kwamba kila nyumba na mitaa ilichukuliwa majira ya nukta kwa ajili ya kuwaongoza makarani wakati wa kuhesabu watu.

"Wakati wa kuhesabu watu, kila mkuu wa kaya alikuwa anataja mali ambazo familia yake inamiliki kwa lengo la kutambua hali ya kiuchumi ya kaya husika na kumbukumbu hizo zikahifadhiwa sambamba na zile picha za satelaiti," alisema Makinda.

Alisema linapotokea janga la asili ambalo linaharibu makazi na kupoteza kumbukumbu kama ilivyotokea katika Mji wa Kateshi wilayani Hanang hivi karibuni, maofisa wa serikali wanatumia taarifa hizo kudhibitisha mali za watu kwenye eneo husika wakati wa kufanya tathmini.

"Wakati wa kufanya tathmini ya athari za janga la kule Hanang, kuna watu walikuwa wanataka kutoa taarifa za uongo ili wanufaike, kwa mfano kunamtu alisema alikuwa na nyumba ya kisasa lakini tuliporejea kwenye picha ya satelaiti na taarifa alizozitoa wakati anahesabiwa kwenye sensa ya mwaka 2022 tukabaini kuwa madai yake ya kwamba alikuwa na nyumba ya kisasa siyo ya kweli," alisema Makinda na kuongeza.

"Mtu mwingine alisema kwamba alikuwa na ng'ombe 50 lakini alipofuatiliwa kwenye taarifa alizotoa wakati anahesabiwa, ikabainika alikuwa na ng'ombe watatu pekee, kwahiyo hii imesaidia sana kupata uhalisia wa mali za wakazi wa eneo hilo," alisema.

Alisema kuwa hata likatokea janga lingine mahali popote nchini, matokeo hayo bado yanaweza kutumika kupata uhalisia wa mali, makazi na hata mifugo iliyoathirika.

Meneja wa NBS wa Mkoa wa Mbeya, John Lyakurwa, alisema mafunzo kwa waandishi wa habari ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya sensa hiyo.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo kwa waandishi wa habari ni kuwajengea uwezo katika kuchambua na kutafsiri matokeo ya sensa ya watu na makazi ili watekeleze majukumu yao kwa weledi zaidi ikiwamo kuelimisha jamii.

Vilevile alisema mafunzo hayo yana lengo la kuwaelimisha wanahabari kuhusu matumizi sahihi ya matokeo ya sensa ikiwamo takwimu mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka waandishi wa habari walioshiriki kwenye mafunzo hayo kuzingatia matumizi sahihi ya taarifa hizo za sensa.

Pia, aliwaomba watumie vizuri taaluma yao kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matokeo ya sensa.



Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi na Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda (kulia), akifuatilia mafunzo ya uwasilishaji, usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe yaliyohitimishwa jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Moto wateketeza bweni la wanafunzi Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI 100 kutoka Shule ya Sekondari Maguvani iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, wamenusurika kifo baada ya bweni lao kuteketea kwa moto usiku.

Moto huo umeteketeza vitu mbalimbali vilivyokuwamo kwenye bweni hilo ikiwamo madaftari, nguo, vitanda na magodoro hali ambayo imesababisha hasara.

Bweni hilo linamilikiwa na kikundi kiitwacho raha na matatizo (KIRAMA) ambacho kimelikodisha kwa wazazi kwa ajili ya wanafunzi hao ili kuondoa adha ya kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni.

Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Mji wa Makambako, Aderick Nombo, alisema tukio hilo lilitokea Januari 28 majira ya saa mbili usiku.

Alisema licha ya wanafunzi wote kuwa salama lakini vifaa vyao hasa madaftari, nguo, mabegi na magodoro vimeteketea kwa moto.

Mkuu wa shule hiyo, Tudeni Mahenge alisema bweni hilo lilikuwa na uwezo wa kulaza wanafunzi 100.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Sekondari Kata ya Maguvani, Nsangalufu Mwakasumbula, alisema chanzo cha moto huo bado hakijafahamika kutokana na bweni hilo kutumia umeme wa jua.

"Wakati mwengine tulikuwa tunafikiri ni umeme lakini bweni lililoungua linatumia sola sasa sijajua sola inaweza kupigisha shoti pale, tunaomba utaalamu wa uchunguzi pengine mtu alienda akachoma sijui," alisema Mwakasumbula.

# Mbaroni tuhuma utapeli, kughushi nyaraka za serikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Pius Komba (70) mkazi wa Itigi jijini Mbeya kwa tuhuma ya utapeli na kughushi nyaraka mbalimbali za serikali na taasisi za umma zikiwamo za mifuko ya hifadhi ya jamii.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali wanazozifanya mkoani hapa.

Alisema mzee huyo alikamatwa Januari 25 mwaka huu wakati maofisa wa jeshi hilo waliposhirikiana na maofisa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambayo ni miongoni mwa taasisi ambazo alikuwa anaghushi nyaraka zake.

Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo ni kinara wa kuandaa nyaraka feki na mihuri ya NSSF na kuwapatia wanachama wa mfuko huo ili wapate mafao yao jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

"Mtuhumiwa alikamatwa katika eneo la Retco jijini hapa ambapo ndipo amekuwa akifanyia shughuli zake hizo, amekuwa akichonga mihuri na kuandaa nyaraka mbalimbali za wastaafu," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema mtuhumiwa amekuwa akishirikiana na baadhi ya wanachama wa mfuko huo na baadhi ya maofisa rasilimali watu wa kampuni wanazofanyia kazi kufanya udanganyifu wa taarifa zinazohitajika ili kulipa mafao kwa mujibi wa sheria.

Alisema katika siku za hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la vishoka ambao wamekuwa wakiandaa nyaraka za kughushi ambazo hutengeneza na kuwapa wanachama wa mfuko kwenda kufungua madai ya mafao.

Katika hatua nyingine, Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili akiwamo raia wa Rwanda aitwaye Assouman Gahigiro (48) kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi zenye uzito wa kilogramu 20.

Kamanda Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo pamoja na mwenzake Winny Bruno (31) mkazi wa Kiwira wilayani Rungwe walikamatwa Januari 27 katika kizuizi cha Kayuki kilichopo kwenye Barabara ya Kyela-Tukuyu wakati wakisafirisha dawa hizo. Alisema watuhumiwa walikuwa wanasafirisha bangi hizo kutoka wilayani Kyela kwenda jijini Mbeya ambako ndiko wanakouza na kwamba walikuwa wameiviringisha kwenye mifuko ya rambo, kisha kuhifadhi kwenye begi la nguo.

Alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji ya Mkoa wa Mbeya linafanya uchunguzi wa uhalali wa Gahigiro kuwepo nchini wakati taratibu zingine za kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wote zinaendelea.



## HABARI ZANZIBAR

# Uhaba wa pombe Zanzibar wawaliza wadau wa utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU wa sekta ya utalii visiwani Zanzibar wamesema uhaba wa pombe uliojitokeza umeanza kuathiri maendeleo ya sekta hiyo pamoja na kampeni ya kuwavutia watalii iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Waliyasema hayo juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti katika ukanda wa utalii wa Paje, Kiwengwa na Nungwi kuhusu uhaba wa pombe uliopo visiwani hapo.

Mohamed Othman kutoka Hoteli ya Nungwi alisema ni jambo la kusikitisha kuona serikali inatumia nguvu kubwa kuvutia watalii, lakini watalii hao wanapokuja Zanzibar wanakosa huduma za vinywaji hususani pombe zinazozalishwa nchini.

"Watalii wamekuwa wakituambia wanahitaji pombe zinazozalishwa nchini na siyo kutoka nje ya nchi, kwao siyo pombe ngeni wanataka kitu chenye ladha tofauti," alisema Mohamed.

Meneja wa Hoteli ya Paje by Night, John Michael Mawilo, alisema kwa sasa pombe imegeuka almasi visiwani Zanzibar hasa bia zinazozalishwa Tanzania Bara tangu kuondolewa kwa kampuni zilizokuwa zinatoa huduma hizo.

Alisema awali pombe zilikuwa zikiingizwa na Kampuni ya Sicoch, Kampuni ya One Stop pamoja na Kampuni ya QMB ambazo zinauzoefu mkubwa katika biashara hiyo na tatizo la uhaba wa pombe halikuwepo Zanzibar kabla ya kunyimwa leseni mwaka huu.

"Lazima tufahamu uhaba huu sio Paje tu bali ni Zanzibar nzima, tumeingia katika suala la utalii, mama Samia ametangaza Filamu ya The Royal Tour ili kuwavutia watalii, lakini watalii wanakuja wanakuta hakuna pombe zinazozalishwa nchi kwa kweli ni aibu kubwa na tunarudisha nyuma sekta ya maendeleo ya utalii," alisema.

Hata hivyo alisema ni jambo la kushangaza kampuni zenye historia kubwa, sifa na uzoefu kwenye kampuni hizo zimenyimwa vibali bila ya kuelezwa sababu na kupewa kampuni mpya ambazo hazina sifa na uwezo wake ni mdogo ikiwamo kukosa miundombinu ya maghala, vyombo vya usafiri baharini na magari.

"Wakati umefika Waziri na Bodi ya Vileo wajitokeze na watueleze chimbuko la uhaba wa vileo na hatua gani wanachukua kumaliza tatizo hilo," alisema.

Meneja wa Baa ya Paje, Patrick Thobias, alisema watalii wamekuwa wakifika katika mgahawa wake lakini wanapoulizia pombe na kuambiwa hakuna hulazimika kuondoka jambo ambalo linawapa mazingira magumu katika biashara zao.

Alisema watalii wanapaswa kupewa huduma zote wanazohitaji ili kuwa mabalozi wazuri wa kuitangaza Zanzibar pindi wanaporudi kwao, lakini kitendo cha kukosekana kwa pombe hasa zinazozalishwa ndani ya nchi madhara yake yataonekana katika siku za baadaye.

Kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar ya Mwaka 2020 ni kampuni tatu pekee ndizo zinazopaswa kupewa vibali vya uingizwaji wa vinywaji na wamiliki wa kampuni hizo lazima wawe Wazanzibar na kupewa leseni kila mwaka.



Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa macho mekundu ambapo hadi sasa wapo wagonjwa 455, kisiwani humo. Kulia ni Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya wa wizara hiyo, Salim Slim. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jeshi la Polisi lapokea msaada vifaa vya kisasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Polisi Zanzibar, CP Hamad Khamis Hamad, ameipongeza Kampuni ya Asas Group kwa kulisaidia jeshi hilo vifaa vya kisasa, akisema vitaongeza kasi ya utendaji.

Alitoa pongezi hizo jana katika ukumbi wa Jeshi la Polisi Ziwani mjini Zanzibar baada ya kupokea msaada wa kompyuta 13 zilizotolewa na kampuni hiyo.

Alisema upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika Jeshi la Polisi utaharakisha kufikiwa kwa mageuzi yanayochukuliwa na jeshi hilo katika kuelekea kwenye matumizi ya vifaa teknolojia katika utendaji.

Hamad alisema kompyuta hizo zitaliwezesha Jeshi la Polisi kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wananchi.

Kamishna Hamad alisema hatua ya kampuni hiyo kutoa msaada huo inadhihirisha katika kuunga mkono hatua za mageuzi ya jeshi hilo yanayotekelezwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kwa msaada huu unadhihirisha nia ya dhati ya kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuliimarisha Jeshi la Polisi na kulifanya kuwa la kisasa zaidi," alisema.

Alisema katika ulimwengu wa sasa jeshi hilo linapaswa kubadilika na lifanye kazi kisasa katika kuwahudumia wananchi sambamba na kuwa na vifaa vinavyoendana na mifumo ya kidijitali.

"Mazingira ya utendaji wa Jeshi la Polisi yamebadilika ambapo mwelekeo ni kwenye dijitali, tunawapongeza sana Asas Group kwa hatua hii mliyoichukua," alisema.

Mwakilishi kutoka Kampuni ya Asas Group, Fahad Masoud Ali, alisema kampuni hiyo imetoa vifaa hivyo kwa Jeshi la Polisi ili liendeleze kusimamia amani iliyopo.

Fahad alisema kampuni hiyo inaunga mkono juhudi za Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kuleta maendeleo.

Alisema wataendelea kuunga mkono jitihada za Jeshi la Polisi kwa sababu ndilo lenye kulinda usalama wa raia na mali zao, lakini pia uwepo wa usalama ndiyo unaowezesha kampuni hiyo kufanya biashara hapa nchini.

# Zanzibar kuimarisha mfumo wa haki jinai kwa wafungwa

**Na Rahma Suleimani,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, amesema ofisi yake inaungana na serikali zote mbili katika kuimarisha mfumo wa haki jinai, kwa kuweka mazingira rafiki kwa wafungwa wanaotumikia vifungo gerezani.

Aliyasema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2023, kwa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi visiwani Zanzibar.

Alisema hatua ya kwanza ni kulihamisha Gereza la Kilimani kuwa makao makuu ya Jeshi la Magereza.

Alisema shughuli za Gereza la Kilimani zitahamishiwa katika Gereza la Hanyegwamchana liliopo Mkoa wa Kusini Unguja ambapo ujenzi wake utazingatia mahitaji na huduma muhimu za kibinadamu.

Aidha, Waziri Masoud alisema ipo miradi mikubwa ya maendeleo ambayo inatarajiwa kuwekewa mawe ya msingi na mengine kuzinduliwa na kuwapongeza wakuu wa mikoa, wilaya na watendaji wa ofisi yake kwa kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, Machano Othman Said, alipongeza uamuzi wa kutaka kujengwa ofisi za masheha ambazo zitarahisisha kwa kupata huduma za kijamii katika eneo maalum tofauti na ilivyo sasa.

Mwenyekiti huyo pia aliwataka wakurugenzi wa serikali za mitaa kubuni na kupata miradi mipya ambayo itakuwa ni vyanzo muhimu vya ukusanyaji wa mapato.

Aidha, aliridhishwa na utendaji wa vikosi vya idara maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika masuala mbalimbali ya kiulinzi na kimaendeleo, jambo ambalo limeongeza imani kwa wananchi katika kuviamini vikosi hivyo.



# Dk. Mpango aonya vijana matumizi mabaya mitandao

**Na Adela Madyane, KIGOMA**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amewaasa vijana kutumia vizuri mitandao ya kijamii, huku akiwaonya kutokukubali kutumiwa kisiasa katika kuchochea vurugu kwa kushiriki maandamano yasiyo na tija

Aliyasema hayo katika kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan na maadhimisho ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM), yaliyofanyika jana kitaifa katika viwanja vya Kawawa vilivyopo Manispaa ya Kigoma, Ujiji.

"Vijana mnapaswa kuwa kielelezo cha uadilifu, mlinde mila na desturi, mtumie mitandao ya kijamii kuongeza maarifa, ili kuleta tija na utatuzi juu ya masuala mbalimbali katika jamii na sio kutumia mitandao kuchafuana, kupotosha na kuleta taharuki katika jamii," alisema Dk. Mpango.

Aidha, alisema ni muhimu vijana wakatumia majukwaa rasmi ya mijadala ili kufikisha maoni yao kwa ajili ya kupata suluhu na si kuandamana kwa kuwa sio suluhu kwa kila kitu.

"Uchumi wa dunia umeathirika na ugonjwa wa Covid-19, vita vya pamoja na vita vinavyoendelea ukanda wa Mashariki ya Kati, athari hizi haziwezi kutatuliwa kwa mara moja tena kwa maandamano, vijana msikubali kutumika," alisema Dk. Mpango.

Alisema Rais Samia anataka usawa na watu wote waheshimiane, wawe wastahimilivu na kuepuka migogogro na pale inapobidi suluhu itafutwe mara moja ili kuleta mageuzi ya kukuza nchi na inaendelea kupambana kwaajili ya kutatua changamoto zilizopo.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, alimshukuru Rais Samia kwa kutimiza ahadi yake ya kufungua mkoa huo katika ziara aliyofanya Oktoba 2022 kwa kufanya kuwa kitovu cha biashara na kwamba kwa miaka mitatu wamepokea Sh. trilioni 11.450 zilitotekeleza miradi ya maendeleo.

"Kwanza kuna mradi wa umeme katika Mto Malagrasi eneo la Igamba lenye KW 45.6, kuunganisha umeme mkubwa kutoka Rusumo, kuanzia Nyakanazi mpaka Kidahwe takribani kilomita 280, umeme wa msongo KV 400 utatoka huko mpaka Kigoma na unatarajiwa kukamilika mwezi wa nne, mwaka huu. "Mradi wa SGR kutoka Tabora wenye urefu wa kilomita 506, kujenga reli ya Uvinza-Msongati wenye gharama ya Sh. trilioni 1.74, ukarabati meli ya mafuta ya Mv Sangara, na ujenzi wa meli za mizigo, ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza meli pamoja na kudumisha huduma za afya."

Makamu Mwenyekiti wa UVCCM, Rehemu Simbu, alisema serikali ya awamu ya sita imekuwa kinara cha demokrasia kwa kuimarisha na misingi ya utu, kuhimiza haki, usawa na uongozi bora jambo ambalo linadumisha amani na mshikamo wa taifa letu.

"Juzi chama kimojawapo kuliweza kufanya maandamano ambayo kipindi cha nyuma hayakuweza kuruhusiwa, lakini wamepewa ulinzi wa kutosha na hii inaonesha kuwapo kwa ukomavu wa kidemokraisa katika awamu hii ya uongozi," alisema Simbu.

Mwenyekiti wa UVCCM, Mohammed Kawaida, alimpongeza Rais Samia kwa kutekeleza ilani ya CCM kwa kuhakikisha fedha za miradi ya kimkakati katika sekta za kilimo, elimu na afya zinapatikana.

Aidha, alikabidhi tuzo ya heshima kwa Makamu wa Rais kwa niaba ya Rais pamoja na kutoa Shilingi milioni moja kwa ajili ya kuchukua fomu ya kugombea urais na kwamba watamsindikiza kuchukua fomu wakati ukifika.

# Wapona sikoseli baada ya kupandikizwa uloto

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma imeandika historia ya watoto watatu kupona ugonjwa wa sikoseli baada ya kuwafanyia matibabu ya upandikizaji uloto.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika alibainisha hayo jana alipotoa taarifa rasmi kwa vyombo vya habari ikiwa ni mwaka mmoja tangu hospitali hiyo ifanye matibabu ya upandikizaji uloto kumtibu mtoto mwenye ugonjwa wa sikoseli.

Dk. Chandika alisema watoto hao hawana maradhi ya selimundu tena. Serikali imewekeza zaidi ya Sh. billioni 3.6 kuwezesha huduma hizo ili kuokoa maisha watanzania.

"Leo (jana) ni siku muhimu sana, ninawataarifu watanzania, Afrika na dunia nzima kwa ujumla kwamba watoto tuliyowapandikiza uloto hawana ugonjwa wa selimundu, wana afya njema na vipimo vimethibitisha hawana ugonjwa huo tena," alisema Dk. Chandika.



Aliwashukuru wazazi wa watoto hao ambao ni Grace Hosea (8), Elisha John (11) na Isack Kedmond (10) kwa kuiamini hospitali hiyo na kuruhusu watoto wao kuwa wa kwanza kupokea huduma za upandikizaji uloto.

Matibabu ya upandikizaji uloto yanagharimu kati ya Sh. milioni 55-65. Hata hivyo, utafiti unaonesha kuwa kumhudumia mtoto mwenye selimundu dawa za kupunguza makali ya ugonjwa, fedha hizo zinaweza kukidhi huduma kwa miaka mitano pekee.

"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga Sh. bilioni moja katika bajeti ya mwaka huu wa fedha kwa ajili ya matibabu ya selimundu, hakuna hata mzazi mmoja ametoa fedha, gharama zote zimebebwa na serikali," alisema Dk. Chandika.

Akitoa ushuhuda mtoto Elisha John (11), kwa niaba ya watoto wenzake waliyopokea huduma ya kupandikizwa uloto, alisema changamoto zote alizokuwa nazo zimetoweka.

"Nilikuwa ninapata shida ya kuumwa kichwa, shuleni nilikuwa simalizi mwezi, lazima nitalazwa wiki nzima, sihudhurii vipindi shuleni, tangu nimetibiwa sijasikia maumivu yoyote," alisema.

Kwa mujibu wa mzazi wa Elisha, kumhudumia mtoto mwenye sikoseli ni "kujitoa sadaka", mzazi mmoja alilazimika kuacha kazi ili kuwa karibu na mtoto wao.

Prof. Cornell Uderzo, Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Upandikizaji Uloto kutoka Shirika la Help 3 la Italia, washirika wa hospitali hiyo katika huduma za upandikizaji wa uloto, alisema hitaji la hosteli ni muhimu si tu kwa hospitali hiyo ya Dodoma, bali pia ni protokali ya matibabu hayo.

# Elimu nyumba kwa nyumba yaongeza wanaume kusindikiza wake kliniki

**Na Christina Mwakangale, Aliyekuwa MWANZA**

MGANGA Mfawidhi Kituo cha Afya Bulale, Dk Wambura Wanchoke, kilichopo mkoani Mwanza, amesema elimu endelevu ya afya ya uzazi nyumba kwa nyumba, imechangia kuongeza idadi ya wanaume kuwasindikiza wenza wao katika kliniki ya Baba, Mama na Mtoto.

Amesema katika kipindi cha miezi sita wenza 167 kati ya 1,223 wamehudhuria kliniki ya Baba, Mama na Mtoto katika kituo hicho, kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana.

"Kwa taarifa ambayo tunayo hadi sasa hatujawahi kuwa na kifo cha mama hapa kituoni. Wakati tunaanza ilikuwa ni kliniki ya Mama na Mtoto sasa tumeboresha ni Kliniki ya Baba, Mama na Mtoto," alisema Dk. Wanchoke.

"Sababu mojawapo ni kauli nzuri na lugha nzuri, kwa wateja. Kuboreshwa kwa kujengwa kwa wodi ya wazazi, chumba cha upasuaji, huduma ya mionzi na huduma ya maabara na wahudumu ngazi ya jamii na kutoa elimu," aliongeza Dk. Wanchoke.

Alisema mwaka 2018 kituo hicho kilikuwa ni zahanati na kupatia hadhi ya kituo cha afya mwaka jana, akisema kwa mwezi Julai mwaka jana, 189 walihudhuria kliniki hiyo kati yao wenza ni 36 na pia Agosti mwaka huo pia 168 walifika kliniki na 19 wakiwa ni wenza.

"Septemba mwaka jana walihudhuria 184 na 19 ni wenza, kadhalika Oktoba mwaka jana 147 walifika kliniki na kati yao 36 walikuwa wenza. Novemba mwaka jana walifika kliniki 314 kati yao ni wenza 28," alisema Dk. Wanchoke

Kwa mwezi Desemba, mwaka jana, Dk. Wanchoke alisema waliohudhuria kliniki ni 221 na kai ya hao 29 walikuwa ni wenza.

Mwalimu Kasase Kulusanga, mkazi wa Bulale, Kata ya Buhongwa, alisema mahudhurio ya kliniki pamoja na mwenzi wake ni jambo la kawaida na hupewa kipaumbele kwa kupatiwa huduma na watoa huduma, kila anapofika kliniki.


**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**LABAN ABAS MAPABHA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE510106** ambayo imetolewa uhamiaji makao makuu uhamiaji **08/09/2022**

(Substituted Service)
IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA AT KAHAMA
LAND APPLICATION No. 128....2023
MAPAMBANO MAYALA..............APPLICANT
VERSUS
MUHOJA MATONGO & ANOTHER........RESPONDENT

TO: JOYCE MASHIMILA

**TAKE** notice that the above matter is coming for Mention on 30 Day of 01 2024 at 09:00 am Before Hon. KAPINGA A.M Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in person or by Advocate or agent dully authorized when the case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and the **SEAL** of this tribunal this 10 day of 01..2024

CHAIRMAN

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**NILAM HASHAM NANJI** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE127585** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 24/06/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/60223/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SAMUEL SULE NAKEI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T 476 EAF** aina ya gari **NISSAN ATLAS** Iliyotolewa na TRA Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa kumb Na. **PHQ/DAR/ILA/13519/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SINDA SAMSON MSETI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari ya aina **TRAILER** yenye usajili namba **T 824 DXU** na CHASSIS NAMBA: **SDCCS45B3AAA33140.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/MAR/TAR/610/2024**

HABARI MCHANGANYIKO

## Nigeria yazikosoa Mali, Niger na Burkina Faso kujiondoa ECOWAS

**ABUJA,** NIGERIA

NIGERIA imesema kwamba viongozi wa kijeshi wasiochaguliwa na raia wa Niger, Mali na Burkina Faso wamewasaliti watu wao kutokana na uamuzi wa pamoja wa kujiondoa kwenye Shirika la Kiuchumi la Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS).

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Nigeria ambayo ni mwenyekiti wa sasa wa ECOWAS, ilizungumza kwa mara ya kwanza baada ya mataifa hayo kutangaza kujiondoa kwenye shirika hilo, ambalo limekuwapo kwa karibu miaka 50.

Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Nigeria kupitia taarifa iliyotolewa jana, alisema kwamba wale wanaokusudia kujiondoa ECOWAS, hawafanyi hivyo kwa nia njema.

"Badala yake viongozi ambao hawajachaguliwa wameamua kuhujumu haki ya wananchi ya uhuru wa kutembea, kufanya biashara, pamoja na kuchagua viongozi wao," alisema.

Ilibainishwa kuwa hadi sasa ECOWAS haijatoa taarifa yoyote kutokana na tangazo la kujiondoa kwa mataifa hayo. Huku Nigeria ikieleza kwamba ipo tayari kushauriana na mataifa yote matatu kuhusu suala hilo.

**VOA**

# Afungwa jela kwa kuvujisha siri za serikali

**ISLAMABAB,** PAKISTAN

ALIYEKUWA Waziri Mkuu wa Pakistan, Imran Khan, amehukumiwa kifungo cha miaka 10 jela katika kesi ambayo alishtakiwa kwa uvujaji wa siri za serikali.

Khan, ambaye alitimuliwa na wapinzani wake kama waziri mkuu mwaka 2022, tayari anatumikia kifungo cha miaka mitatu jela baada ya kupatikana na hatia ya ufisadi, ikibainishwa kuwa mashtaka yote dhidi yake ni ya kisiasa.

Inaelezwa kuwa hukumu hiyo chini ya sheria ya siri imekuja wiki moja kabla ya uchaguzi mkuu ambao amezuiwa kugombea.

Aidha, ilibainishwa kwamba Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Shah Mahmood Qureshi na Makamu Mwenyekiti wa chama cha Khan cha Pakistan Tehreek-e-Insaf (PTI) pia walihukumiwa kifungo cha miaka 10 jela na mahakama maalum.

Ilielezwa kuwa kinachojulikana kama kesi ya siri inahusu madai ya uvujaji wa barua za siri za kidiplomasia zilizotumwa na balozi wa Pakistan mjini Washington kwenda Islamabad wakati Khan alipokuwa waziri mkuu.


Inahusiana na kuonekana kwake katika mkutano wa Machi 2022, mwezi mmoja kabla ya kuondolewa mamlakani kwa kura ya kutokuwa na imani naye. Ikielezwa kuwa Khan pia alionekana jukwaani, akipunga karatasi ambayo anasema ilionyesha njama za kigeni dhidi yake.

Alisema ilieleza kwa kina kwamba wote watasamehewa ikiwa Khan ataondolewa madarakani japokuwa hakutaja nchi hiyo licha ya kwamba aliikosoa sana Marekani.

Upande wa mashtaka ulisema kwamba hatua za Khan ni sawa na kuvujisha waraka wa siri na kuharibu uhusiano wa kidiplomasia. Ikielezwa kuwa shtaka la mwisho linaweza kusababisha kifungo cha maisha au hata adhabu ya kifo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kesi hiyo imesikilizwa kwa muda wa miezi michache iliyopita ndani ya mahakama maalum iliyoundwa ndani ya jela ambayo Khan amekuwa akishikiliwa tangu Agosti, 2023.

Chama cha Khan cha PTI kilisema kitapinga uamuzi wa mahakama na kuuita dhihaka. Na kwamba uchaguzi mkuu utafanyika Februari 8, mwaka huu, huku kukiwa na madai kuwa PTI inazuiwa na mamlaka kufanya kampeni. **BBC**



Wahudumu wa afya wakitoa chanjo ya ugonjwa wa kipindupindu kwa wakazi wa wilaya 26 zilizoathirika nchini Zimbabwe. **PICHA: AFP**

# CRDB yapata faida ya bilioni 424/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetangaza matokeo ya kifedha kwa mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2023, ikionesha imepata faida ya mabilioni ya shilingi.

Taarifa hiyo ya fedha ambayo haijakaguliwa iliyotolewa jana, imetangaza faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 424, ikiwa ni ongezeko la asilimia 21 kulinganisha na mwaka jana.

Taarifa hiyo ya fedha inaonesha ukuaji mkubwa katika viashiria muhimu vya utendaji. Jumla ya rasilimali imeongezeka kwa asilimia 14 kutoka Sh. trilioni 11.6 hadi Sh. trilioni 13. Amana za wateja zimeongezeka kwa asilimia nane kufikia Sh. trilioni 8.9, wakati mikopo imeshuhudia ukuaji mkubwa wa asilimia 23 kufikia jumla ya Sh. trilioni 8.5.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alieleza kufurahishwa na utendaji wa benki hiyo, akisema "Tuna furaha kutangaza mwaka mwingine wa ukuaji mkubwa na kuimarisha nafasi yetu katika sekta ya fedha nchini. Matokeo haya yanaonesha dhamira yetu katika kujenga benki imara na kutoa thamani endelevu kwa wadau wetu."

Nsekela alisisitiza kuwa utekelezaji wa mkakati mpya wa muda wa kati wa benki hiyo (2023 - 2027) umekuwa chachu ya kufikia matokeo yaliyovunja rekodi yake.

Alisisitiza "utekelezaji thabiti wa mipango yetu ya kimkakati umekuza ukuaji wa kipekee, unaothibitishwa na ongezeko la asilimia 35 ya mikopo kwa biashara ndogondogo na za kati, na maendeleo makubwa katika ufadhili jumuishi katika sekta na makundi mbalimbali kama vile vijana na wanawake, kilimo na ufadhili endelevu."

Uwekezaji wa kimkakati wa benki katika mabadiliko ya kidijitali unaleta faida kubwa, ikidhihirishwa na ukuaji wa asilimia 11 katika mapato yasiyo ya riba, yanayochangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za kidijitali.

Nsekela alisisitiza, "kujitolea kwetu katika kubuni suluhisho za ubunifu kwa ajili ya kuboresha maisha ya wateja wetu na uchumi, kama ilivyo katika huduma bunifu ya bima nafuu kwa bodaboda na bajaji 'Bima ya Buku', kumeimarisha utendaji wetu wa kifedha kwa ujumla."

Fredrick Nshekanabo, Ofisa Mkuu wa Fedha, aliangazia uimara wa kifedha wa benki hiyo, akisema, "mtazamo wetu katika kuimarisha huduma za mikopo unadhihirika katika uwiano wa mikopo chechefu wa asilimia 2.8.

"Uwiano wa gharama na mapato umeendelea kuwa katika kiwango cha udhibiti pamoja kwa kufikia asilimia 49.5 pamoja na kuongezeka gharama za uendeshaji iliyosababishwa na kuzorota kwa mazingira ya uchumi mpana kimataifa."

Utendaji mzuri wa benki umepelekea faida kubwa ya asilimia 26.7 kwenye mapato ya hisa, ikiambatana na ongezeko la asilimia 14 la bei ya hisa na kufikia Sh. 460 kwa hisa hadi tarehe 31 Desemba 2023.

Benki ya CRDB pia imeendelea kuimarisha mtaji wake, ikijivunia uwiano wa utoshelevu wa mtaji ambao unazidi kwa kiasi kikubwa mahitaji ya udhibiti.

Katika mwaka uliopita, Benki ya CRDB ilipanua wigo wake wa kutoa huduma kwa kuanzisha kampuni tanzu za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na kuingia katika sekta ya bima kwa kuanzisha kampuni ya Bima ya CRDB.

Hatua hizo za kimkakati zinaimarisha zaidi wigo wa benki hiyo si tu Tanzania bali pia katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki.

Vilevile, kuanzishwa kwa taasisi ya CRDB Bank Foundation kunasisitiza dhamira ya Benki ya CRDB kupanua ushiriki wake katika jamii na mipango yake ya uwezeshaji husasan kwa wanawake na vijana, ikionesha azma yake ya kuleta matokeo chanya zaidi ya huduma za kibenki zilizozoeleka.

Nsekela alisema, "Benki ya CRDB imejipanga vyema kwa siku zijazo, na tunajidhatiti kutoa thamani endelevu kwa wateja wetu, wanahisa na jamii tunazohudumia. Mtazamo wetu katika ukuaji endelevu utaendelea kuongoza uamuzi wetu wa kimkakati katika miaka ijayo."

HABARI MICHEZO

# ADAM ADAM WA MASHUJAA KUJITANGAZA MECHI YA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA kinara wa Mashujaa FC, Adam Adam, ameionya Simba kuwa isitarajie mechi rahisi Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, huku akibainisha kuwa kwake itakuwa ni mechi ya kujitangaza.

Akizungumza jijini Dar es Salaam ambako imeweka kambi kujiandaa na urejeo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyokuwa imesimama kupisha Kombe la Mapinduzi na Fainali za Mataifa ya Afrika, straika huyo ambaye ameshawahi kuzichezea Prisons na JKT Tanzania, alisema mbali na kwamba kama timu wanakwenda kupambana na timu kubwa ya Simba, lakini kwake binafsi pia itakuwa ni fursa ya kuonyesha kile ambacho amejaliwa kwa sababu anaamini mechi hiyo itatazamwa na mashabiki wengi.

„Mimi hii ndiyo kazi yangu nikiamka asubuhi akili yangu ni kwenye kazi hii, lengo ni kupambana kulinda nafasi yangu, nataka nifunge mabao na nipate riziki, halafu pia niweze kujitangaza na kupata klabu bora zaidi itakayonipa maslahi mkubwa zaidi, kama ikipatikana fursa kama hii ya kuangaliwa na watu wengi zaidi itumie," alisema straika huyo mwenye mabao matano mpaka sasa kibindoni.

Akizungumzia maandalizi ya mechi hiyo alisema yamekuwa ya nguvu na kwamba kwa asilimia kubwa walikuwa wakifanya maandalizi ya mechi zote za Ligi Kuu na si kuangalia mechi moja tu kwa sababu muda mrefu walikuwa kwenye mapumziko.

„Naamini utakuwa mchezo mzuri na kwangu ni mechi ya kuonyesha kile nilichonacho, tunaenda kukutana na Simba tutaiheshimu kwa ukubwa wake, lakini tutashindana nao kimpira, hakuna kingine na hakuna maneno mengi," alisema.

Kuhusu kutofanya vema kwenye mechi za ligi mpaka sasa, Adam alisema ni upepo mbaya uliwapitia, lakini anadhani hali itarudi kawaida.

„Mwanzoni tulianza vizuri, lakini katikati hapo upepo ukabadilika tukaanza kupoteza mechi, nadhani kwa sasa tumeongeza wachezaji, tutafanya vema," alisema.

Mashujaa FC inashika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi tisa kwa mechi 12 ilizocheza.

JEZI...



Katibu Tawala Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Mohamed Mfaki, akimkabidhi seti moja ya jezi na mpira mmoja Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Bonde wilayani hapo, Grace Killiwe, kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA, katika hafla iliofanyika ofisi ya mkuu wa wilaya, ambapo seti za jezi 34 na mipira 34 zenye thamani ya Sh. milioni 15 zilitolewa katika shule zote 34 za sekondari za serikali wilayani hapo. Kushoto ni Katibu wa mbunge wa jimbo hilo, Omari Kidundai na katikati ni Diwani wa Kata ya Tanganyika, Shafii Chewaja. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mgosi alia ratiba Ligi soka la Wanawake

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI maafande wa JKT Queens wakiongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Soka Wanawake nchini, Kocha Mkuu wa timu ya Simba Queens, Mussa Hassan Mgosi, ameilalamika ratiba kuwa siyo rafiki kwao kwani wamekuwa wakisafiri kwa muda mrefu na wachezaji wake kukosa nafasi ya kupumzika.

Licha ya Jumamosi iliyopita kupata ushindi wa mabao 7-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam dhidi ya Alliance Girls, Mgosi amesema kwa upande wao ratiba haijawatendea haki kwani mechi za awali kabla ya hiyo wamelazimika kusafiri mikoa ya mbali, kitu ambacho kinawachosha sana wachezaji wake.

„Tumecheza mechi hii tukitokea mkoani Mara kucheza na Bunda Queens, kabla ya hapo tulikuwa mkoani Lindi kucheza na Amani Queens na sasa ratiba inaonyesha kuwa tunatakiwa kutoka tena, hii kwetu haijakaa vizuri wakati wenzetu wao wanapumzika sana," alisema Mgosi.

Simba Queens ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 16, ikiongozwa na JKT Queens iliyo kileleni na pointi 18.

Suluhu iliyoipata Simba Queens dhidi ya Bunda Queens kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara, Januari 22, ndiyo iliyoifanya timu hiyo kuzidiwa pointi mbili dhidi ya vinara.

Cessia Queens ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 13, Yanga Princess ya nne na pointi zake 12, huku Fountain Gate Princess ikiwa nafasi ya tano, ikikusanya pointi nane.

Timu ya Bunda Queens yenyewe inakamata nafasi ya sita ikiwa na pointi nane pia, Baobab Queens ya saba pointi zake saba, Amani Queens nafasi ya nane ikiwa na pointi sita, Alliance Girls ya tisa na pointi zake sita, huku timu ya Geita Queens ikiburuza mkia ikiwa na pointi moja tu.

Timu sita zimecheza mechi saba mpaka sasa na nne ambazo ni Mabingwa Watetezi, JKT Queens, Simba Queens, Fountain Gate Princess pamoja na Amani Queens zikiwa zimecheza mechi sita tu.

## Fountain Gate FC yaleta mtaalamu kutoka Denmark

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa katika timu ya wakubwa, uongozi wa Taasisi ya Fountain Gate, umeanza kutupia jicho lake la tatu katika kuendeleza soka la vijana wanaume na wanawake kwa kumleta mtaalamu Frank Petersen kutoka Denmark kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa timu hizo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo, Calvin Shaban, alisema wamekuwa na utaratibu wa kuunganisha wachezaji kutoka katika timu zao kwenda kucheza soka la kulipwa katika mataifa mbalimbali.

Alisema katika mwendelezo huo wamefanikiwa kuingia makubaliano na Kocha Petersen kwa ajili ya kuja nchini kutoa mafunzo na kuandaa programu kwa timu zao za vijana na wanawake kwa lengo la kuwapa ujuzi.

"Tumeamua kuwawezesha vijana wetu kwa kuleta mtaalamu kuja kutoa mafunzo kwa walimu wetu wa soka la vijana na wanawake, atakuwapo mchini kwa muda wa wiki mmoja, kwa mwaka atakuja mara tatu hadi tano kwa ajili ya mafunzo hayo.

„Lakini mbali na mafunzo pia atakuwa sehemu ya kuwatafutia nafasi wachezaji wetu hasa vijana na wanaocheza soka la wanawake kwenda nje kutafuta changamoto nyingine," alisema Calvin.

Aliongeza kuwa mtaalamu huyo mwenye uwezo wa kufundisha makipa pia, atapata nafasi ya kutembelea timu na kutoa mafunzo kwa makipa wa timu yao ya Singida Fountain Gate FC ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa upande wa mtaalamu huyo, alisema yupo nchini kwa ajili ya kutoa mafunzo na kuongeza ujuzi kwa taasisi hiyo kwa kutoa elimu kwa makocha, wachezaji ikiwamo soka la vijana na wanawake.

"Nina uzoefu wa muda mrefu, nimekuja kutoa mafuzo kwa vijana na kuendeleza soka la wanawake kwa kutoa elimu ya soka, lakini kuwapa nafasi ya kwenda nje kuwatafutia timu na kucheza soka la kulipwa," alisema Petersen.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OLISE ANAITAKA UNITED
CHELSEA ina nia ya kumsajili Michael Olise wa Crystal Palace msimu huu, lakini winga huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, anapendelea kuhamia Manchester United. **(Football.London)**

### LIVER KIBARUA KIGUMU
KLABU ya Liverpool itakabiliana na kibarua kigumu cha kuwapata makocha wanaolenga ili kupata kocha wa kurithi mikoba ya Jurgen Klopp msimu huu, huku Xabi Alonso akifuatiliwa na Bayern Munich na Roberto de Zerbi wa Brighton akilengwa na Manchester United iwapo watamfuta kazi Erik ten Hag. **(Telegraph)**

### ALONSO KUBAKI LEVERKUSEn
KLABU ya Bayer Leverkusen ina uhakika Xavi Alonso atasalia katika klabu hiyo msimu huu licha ya klabu yake ya zamani ya Liverpool kumtaka. (Sky Germany)

### BENRAHMA ATAKIWA EVERTON
EVERTON inafikiria kumnunua kwa mkopo winga wa West Ham raia wa Algeria, Said Benrahma mwenye umri wa miaka 28. **(HITC)**

### ESTEVE APANDIWA DAU
KLABU ya Burnley imetoa dau la pauni milioni 10.2 kumnunua beki wa kati wa Montpellier mwenye umri wa miaka 21, raia wa Ufaransa, Maxime Esteve. **(Mail)**

### CHOLABAH AFIKIRIWA FOREST
KLABU za Nottingham Forest, West Ham na Fulham zinafikiria kumnunua beki wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24, Trevoh Chalobah. **(Football Insider)**

### ROBERTS ATAKIWA LEEDS
KLABU za Brentford, Feyenoord na Leeds United zinavutiwa na beki wa kulia wa Burnley, Conor Roberts mwenye umri wa miaka 28. **(Mail)**

### HOJBJERG AWINDWA LYON
LYON bado inavutiwa na kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28 na mshambuliaji wa Villarreal, Arnaut Danjuma (26), ambaye yuko kwa mkopo Everton. **(L'Equipe)**

### SENSI NA LEICESTER
KLABU ya Leicester imetoa ofa ya kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan, Stefano Sensi mwenye umri wa miaka 28, kwa mkopo na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu ikiwa watapanda Ligi Kuu England. **(Gianluca di Marzio)**

### ALMIRON ATAKIWA AL-SHABAB
KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Shabab bado inavutiwa na winga wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 29 kutoka Paraguay, Miguel Almiron. (Mail)

### RONALDO NA SWANSEA
KLABU ya Swansea inakaribia kumsajili winga wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, Ronald kutoka Gremio Anapolis. **(Wales Online)**

### GODFREY KWA MKOPO
LEEDS United imewasiliana rasmi na Everton kwa ajili ya kumsajili beki wa England mwenye umri wa miaka 26, Ben Godfrey kwa mkopo. **(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KOCHA WA IVORY COAST ASEMA HAKUNA KULALA

●●● Hatupaswi kuishia hapa, lazima tuendelee kufanya kazi, kudumisha ari hii na...

**YAMOUSSOUKRO, Ivory Coast**

KOCHA wa muda wa Ivory Coast, Emerse Fae, amesema timu yake „lazima isiishie hapa" baada ya ushindi wao mkubwa wa mikwaju ya penalti dhidi ya Senegal katika hatua ya 16 bora ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), Jumatatu.

Wenyeji wa michuano hiyo waliwaondoa mabingwa hao watetezi kwa mikwaju ya penalti 5-4 Jumatatu usiku kutokana na sare ya bao 1-1 baada ya muda wa ziada na kutinga robo fainali.

Mbele ya umati wa mashabiki wao kwenye Uwanja wa Charles Konan Banny, Yamoussoukro, Senegal walianza kwa furaha na kuchukua uongozi dakika nne pekee.

Krosi nzuri sana kutoka kwa Sadio Mane ilimpata Habib Diallo, ambaye alipiga mkwaju kwa utulivu na kuandika bao.

Ivory Coast waliamka na kusukumiza mashambulizi hadi dakika ya 86 ambapo wenyeji walipewa penalti baada ya Pepe kuangushwa na golikipa, Edouard Mendy.

Baada ya VAR kukagua tukio hilo, Franck Kessie alimfunga Mendy mkwaju huo wa penalti na kusawazisha bao.

Katika mikwaju ya penalti, Kessie alipiga hatua na kukwamisha mkwaju wa ushindi na kuwafanya watu wa nyumbani kushangilia.

Ilileta mabadiliko makubwa kwa 'Tembo' hao baada ya mchuano mbaya wa makundi kuwashuhudia wakipata vipigo viwili, ikiwa ni pamoja na kufungwa mabao 4-0 na Equatorial Guinea.

"Tulikuwa na mwanzo mgumu, tukiruhusu bao la mapema, lakini niliwaambia wachezaji wakati wa mapumziko waendelee kucheza hivyo hivyo, wasichanganyikiwe," alisema Fae mara baada ya mchezo huo.

Tofauti na chini ya kocha wa awali, Jean-Louis Gasset, Fae alichukua jukumu kamili la maamuzi ya kimbinu wakati wa mechi.

„Ulikuwa uamuzi wangu juu ya kile kinachohitajika kufanywa. Nikiwa na Gasset, ningetoa maoni na angefanya uamuzi," Fae alieleza.

Bosi huyo wa muda alikiri kuwa alikuwa chini ya shinikizo kubwa kabla ya mechi dhidi ya Senegal.

„Kulikuwa na shinikizo kubwa kabla ya mechi, na siku ya mechi ilikuwa ndefu sana kwangu. Sikuweza kulala kama kawaida, nikifikiria matukio yote. Nikisema hakuna shinikizo, nitadanganya," Fae alikiri.

Lakini kuvuka hatua ya makundi kuliongeza imani kabla ya kuwakabili mabingwa hao.

„Kufuzu baada ya ushindi wa Morocco kulitupa kujiamini. Tuliwashinda Senegal na kuwaondoa; morali ni nzuri," alisema Fae.

Huku wakiwa wamefuzu kwa robo fainali, Fae alisisitiza kuwa timu haiwezi kubebwa na matokeo haya kwani majaribio magumu zaidi yanatarajiwa.

„Hatupaswi kuishia hapa; lazima tuendelee kufanya kazi, kudumisha ari hii, na kuendelea kucheza mechi baada ya mechi," alisisitiza.




# ‘CAPE VERDE INA MENGI YA KUTHIBITISHA’

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KIUNGO wa kati wa Cape Verde, Jamiro Monteiro, amesema kikosi chao kina zaidi ya kuthibitisha kufuatia kufuzu kwa robo fainali ya michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), juzi.

Monteiro aliibuka kuwa mchezaji bora wa mechi baada ya kusaidia nchi yake kurekodi ushindi mdogo dhidi ya Mauritania.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Monteiro alisisitiza Cape Verde wana zaidi ya kuthibitisha na watatoa kila kitu kama timu katika michezo inayofuata.

„Ningependa kutoa tuzo hii kwa Cape Verde na kwa watu wote wanaotuunga mkono. Inapendeza sana, tumepiga hatua nyingine mbele, lakini bado hatujaonesha kila kitu. Bado tunaweza kufanya mengi, lakini zaidi muhimu ni kufuzu kwa robo fainali,“ alisema Monteiro.

Monteiro alitangulia kumsifu mfungaji mabao, Ryan Mendes kwa sifa zake za uongozi.

„Yeye ni mfano wetu wa kuigwa. Niko hapa na ninaweza kukuambia ni kiongozi mkuu,“ aliongeza.

# Arteta akasirishwa kutajwa Barca

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amepuuzia mbali uvumi kuwa anaweza kuondoka Arsenal na kujiunga na Barcelona mwishoni mwa msimu huu na kusema ni „habari za uwongo“ na „nimechukizwa“ na ripoti hizo.

Ripoti kutoka Hispania Jumapili zilidai kuwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 41, alikuwa tayari kumrithi Xavi katika klabu hiyo pale Spotify Camp Nou, ambako alipitia akademi ya vijana ya klabu ya La Masia akiwa kijana.

Vyanzo vingi viliiambia ESPN kwamba Arteta anaendelea kujitolea kikamilifu kwa Arsenal, na alionesha msimamo huo kabla ya safari ya timu yake ya Ligi Kuu ya England dhidi ya Nottingham Forest.

„Hizo ni habari za uwongo kabisa,“ alisema Arteta katika mkutano na waandishi wa habari jana alipoulizwa kama ataondoka. “Ulichosoma jana sijui kinatoka wapi, na si kweli kabisa, nimesikitishwa sana nacho.

„Sikuweza kuamini. Sijui inatoka wapi na haina chanzo. Haina chochote, na nadhani tunapaswa kuwa waangalifu sana unapozungumza juu ya mambo ya binafsi ili kuiweka jinsi ilivyowekwa jana.

„Nipo mahali sahihi, nipo na watu sahihi, najisikia vizuri sana. Kama nilivyosema mara nyingi, nimewekeza katika safari nzuri na klabu hii ya soka, na wachezaji hawa, wafanyakazi hawa, watu wetu, na bado kuna mengi ya kufanya.

„Ninakuwa mwangalifu sana ninapozungumza hadharani juu ya mambo yangu ya binafsi, na mtu anapoweka taarifa ya kusema kitu nilichosema au kufanya, inasikitisha.

„Ninaelewa tuko kwenye tasnia hii, lakini nadhani hakuna mtu anayestahili kusikia katika habari kama hiyo na nimekuwa nikiwa sawa na kusema kinyume kabisa, ndiyo maana nimekasirika.“

Arteta alitumia miaka mitatu kama kocha msaidizi chini ya Guardiola kabla ya kuchukua hatua yake ya kwanza ya usimamizi na Arsenal mnamo Desemba 2019.

Wakati kiungo huyo wa zamani wa Arsenal na Everton aliposhinikizwa iwapo angeweza kuinoa klabu nyingine nchini England, Arteta alisema: „Leo, hapana. Lakini sijui. Nilichezea klabu mbili katika nchi hii. Mimi ni mdogo sana na sijui kitakachotokea.“



## Rashford, Ten Hag wayamaliza

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford amefanya mazungumzo ya wazi na kocha Erik ten Hag kuelekea mechi ya Ligi Kuu England ya Manchester United dhidi ya Wolves kesho, Alhamisi.

Ten Hag alizungumza na Rashford pamoja na Mkurugenzi wa Soka, John Murtough na kaka na wakala wa Rashford, Dwaine, baada ya mshambuliaji huyo wa England kupigwa picha akiwa katika klabu ya usiku ya Belfast wiki iliyopita.

Rashford aliombwa kuelezea safari na kufafanua muda wa ziara yake katika mkutano na waandishi wa habari kule Carrington Jumatatu.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo baadaye ilisomeka: „Marcus amechukua jukumu kwa hatua yake. Hili limeshughulikiwa kama suala la ndani la kinidhamu, ambalo sasa limefungwa.“

Siku ya Ijumaa, klabu ilikuwa na hisia kwamba Rashford alikuwa amekwenda klabu ya usiku ya Belfast kabla ya siku iliyopangwa ya mapumziko Alhamisi.

Tangu wakati huo kumekuwa na ripoti kwamba alikuwa huko Alhamisi usiku kabla ya kuwajulisha United alikuwa mgonjwa sana na kushindwa kufanya mazoezi siku ya Ijumaa.

Alikosa mazoezi Ijumaa na Jumamosi na hakuwapo kwenye kikosi kilichoshinda mabao 4-2 dhidi ya Newport County katika Kombe la FA Jumapili. Rashford, ingawa, aliweza kufanya mazoezi huko Carrington Jumapili.

Si mara ya kwanza kwa Rashford kukumbwa na matatizo na Ten Hag baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kuhudhuria sherehe ya kuzaliwa katika klabu ya usiku ya Manchester saa chache baada ya Man United kuchezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Manchester City Oktoba mwaka jana.

Ten Hag alitaja tukio hilo kuwa „halikubaliki“ na Rashford akaomba msamaha. Mshambuliaji huyo wa England alitolewa kwenye mchezo dhidi ya Wolves msimu uliopita baada ya kuchelewa kufika kwenye mkutano wa timu.



HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS KUIWINDA SAUZI KUFUZU OLIMPIKI

**Na Saada Akida**

KUWAPO kwa wachezaji wengi wa Kitanzania wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchini ni moja ya sababu ya kuchelewa kwa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kuingia kambini kujiandaa na michezo ya kufuzu Olimpiki, imeelezwa.

Twiga Stars inatarajia kuingia kambini wiki ijayo tayari kwa maandalizi mechi zake mbili za kuwania kufuzu Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini, utakaopigwa Februari 19 na 28, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema safari hii wamechelewa kuita kikosi kwa sababu kuna mabadiliko kidogo ikiwamo baadhi ya wachezaji kucheza soka la kulipwa nje nchi na ligi katika mataifa hayo zinaendelea.

Alisema kulingana na ratiba za klabu za wachezaji hao kubana, wamelazimka kuchelewa kuingia kambini ambapo Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajiwa kusimama mwishoni mwa wiki hii.

"Baada ya kusimama kwa ligi tutawaita wachezaji kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Afrika Kusini ambao tunaenda kucheza kwao baadaye tutarudiana nyumbani katika Uwanja wa Azam Complex," alisema Shime.

Aliongeza kuwa licha ya kuchelewa kuingia kambini, bado anaimani na wachezaji ambao atawaita katika kikosi chake watafanya vizuri kwenye mchezo huo dhidi ya Afrika Kusini kwa kusaka matokeo mazuri katika michezo yote miwili na hatimaye kusonga mbele.

Shime alisema wanahitaji kufanya vizuri katika michezo hiyo ili kuwa miongoni mwa timu mbili ambazo zitasonga mbele kwenda kuiwakilisha Afrika katika michuano hiyo.

Twiga Stars imefanikiwa kutinga raundi ya tatu ya mchujo wa kuwania tiketi ya Fainali za Michezo ya Olimpiki mwakani jijini Paris, Ufaransa baada ya ushindi wa baada ya kuitoa Botswana.

Tanzania watakuwa ugenini dhidi ya wenyeji hao Afrika Kusini, Februari 19 na 28, mwaka huu, watarudiana katika dimba la Azam Complex , Chamazi, Dar es Salaam.

AFCON...



Kipa wa Misri, Mohamed Gabaski, akiiokoa timu yake kuzama huku washambuliaji wa DR Congo, Meschak Elia (kushoto) na Cedric Bakambu (jezi namba 17), wakiwahi kujiweka tayari endapo atafanya makosa. Katika mechi hiyo ya hatua ya 16 bora ya Fainali za Mataifa ya Afrika iliyopigwa Jumapili usiku nchini Ivory Coast, DR Congo ilitinga robo fainali kwa mikwaju ya penalti 8-7 baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 120. **PICHA: MTANDAO.**

# Kichuya amfunda Chasambi Simba

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa zamani wa Simba, Shiza Kichuya, amemtabiria mchezaji kinda, Ladack Chisambi, kufanya makubwa kama alivyofanya yeye au zaidi, kikubwa akimtaka afanye kilichompeleka kwenye klabu hiyo kubwa na yenye mashabiki wengi.

Kichuya, amesema amefurahi kuona mchezaji mwenzake huyo kinda wa miaka 19, akifuata nyayo zake kwani na yeye alijiunga Simba akitokea Mtibwa Sugar ya Morogoro, akicheza nafasi hiyo ya winga.

„Naamini Chasambi atafanya makubwa Simba, kwa sasa siyo tena timu ya kuungaunga kama ilivyokuwa hapo katikati, tayari naona wameshajipata ila isipokuwa ni suala la muda tu, kwa uchezaji wake naamini atakuwa nyota baadaye, ila yeye mwenyewe tu atulize akili ajue kitu ambacho anatakiwa kukifanya, ajue pia wanachama na mashabiki wa Simba wanahitaji nini, basi atafika pale ambapo anatakiwa kufika,"alisema Kichuya ambaye alipata umaarufu mkuwa akiwa na klabu hiyo mara tu baada ya kujiunga nayo mwaka 2016.

Winga huyo ambaye kwa sasa amejiunga na JKT Tanzania kipindi cha dirisha dogo la usajili akitokea Namungo, alimshauri Chasambi ambaye Mtibwa Sugar ilimpandisha msimu huu kutokea timu ya vijana chini ya miaka 20, kutoweka presha kichwani, au kutaka kufanya mambo makubwa kwa muda mfupi, akiamini hiyo inaweza kumpoteza.

„Ninachomshauri asiweke presha kichwani mwake kwa sababu umri wake na alipoenda ni vitu viwili tofauti, nina maana umri wake mdogo amekwenda kwenye klabu kubwa asianze kujipa ukubwa wakati bado mdogo na hajaipa timu mafanikio yoyote, na asilazimishe kutaka kuibeba timu kwa nguvu, kila kitu kina muda wake.

„Kwa sasa Chasambi anaweza tu kuisaidia Simba kwa sababu ya kipaji chake ila umri wa kuibeba timu mabegani mwake bado hajaufikia, lakini apambane,“ alisema.

Simba ilimsajili Chasambi kipindi cha dirisha dogo la usajili lililofungwa Januari 15 na alianza kuonekana katika mechi chache tu za Kombe la Mapinduzi, visiwani Zanzibar.

## Benchikha kuishushia Tembo straika wapya

INATOKA UK. 24

dhidi ya KMC na kutoka sare ya mabao 2-2.

Mchezo huo tayari umevuta hisia kubwa za wanachama na mashabiki wa timu hiyo, ambao wanataka kushuhudia usajili wao mpya wa dirisha dogo baada ya Benchikha kueleza nia yake ya kuwapa nafasi baadhi ya nyota hao wapya.

Wachezaji wapya waliosajiliwa Simba katika dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu hawakuonekana uwanjani katika michuano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar ni Edwin Balua, Pa Omar Jobe na Freddy Michael Kouablan.

Wapya wa dirisha dogo waliocheza Kombe la Mapinduzi ni Salehe Karabaka, Babacar Sarr na Ladack Chasambi.

Akizungumza na Nipashe, Benchikha alisema anatarajia kufanya mabadiliko madogo huku nyota wapya wakitarajiwa kuonekana katika mchezo wa huo wa leo.

Benchikha alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu hawawafahamu wapinzani wao na wanahitaji kupata ushindi lakini pia atatumia mchezo huo kutengeneza muunganiko wa kikosi chake kwa nyota wapya na walikuwapo awali.

Alisema wanahitaji kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri, lakini kuwapa nafasi wachezaji wapya kuonyesha kile ambacho amewapa katika uwanja wa mazoezi.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu tunacheza na mpinzani hatumfahamu, tutacheza kumheshimu Tembo FC, Simba ni timu kubwa na tunahitaji kuingia na mbinu za ushindi ili kusonga mbele katika hatua inayofuata," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa ni mchezo ambao utakuwa na mabadiliko madogo ya kikosi chake kutokana na wachezaji wao waliokuwa timu za taifa wamechelewa kuungana na kikosi cha timu hiyo katika programu za mazoezi.

Benchikha alisema pia mechi hiyo anaitumia kwa ajili ya kuandaa timu yake kuelekea mechi zinazowakabili za Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwamo dhidi ya Mashujaa FC na Tabora United, ambazo zote watakuwa ugenini.

Naye Kocha wa Tembo FC, Ramadhan Kilobi, alisema wanafahamu Simba ni timu kubwa ndani na nje ya uwanja, lakini hawataingia kinyonge badala yake watapambana kutafuta matokeo mazuri.

Alisema kwa muda mrefu wamekuwa katika maandalizi mazuri ikiwamo mechi za kirafiki dhidi ya Tabora United ambapo walifungwa mabao 3-1, lakini baada ya hapo walirejea mazoezini na kusawazisha makosa yote.

"Tulipoteza mchezo wetu wa kirafiki mbele ya Tabora United, baada ya hapo tukafanyia kazi madhaifu yote ambayo yalionekana na tupo imara kila upande kuhakikisha tunaifunga Simba," alisema.

Michezo
Jumatano Januari 31, 2024
Nipashe

Arteta akasirishwa kutajwa Barca UKURASA 22



DALUGA...



Mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane, akikwepa daluga la winga wa Ivory Coast, Christian Kouame, kwenye mechi ya hatua ya 16-bora iliyopigwa nchini Ivory Coast juzi. Katika mechi hiyo wenyeji walishinda kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya dakika 120 kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SC: GUEDE SI MRITHI WA MAYELE

●●● Yasema sababu kusajiliwa ni Ligi ya Mabingwa na kwamba mabao yapo kwa kina...



**Adam Fungamwango**

LICHA ya wengi kufikiri kuwa Yanga imemsajili mshambuliaji Joseph Guede (pichani), kuja kuziba pengo la Fiston Mayele, ambaye tangu aondoke msimu uliomalizika bado viatu vyake havijapata mtu sahihi, uongozi wa klabu hiyo umesema hakuwa na shida ya mabao kwa sababu wanayapata kwa wachezaji wao uwanjani hasa kwenye Ligi Kuu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema kwa sasa Yanga imeimarika zaidi tofauti na ile ya kocha raia wa Tunisia, Nasreddine Nabi, kwani haimtegemei mchezaji mmoja tu kufunga mabao, badala yake yamekuwa yakifungwa na wachezaji tofauti, hasa viungo washambuliaji.

"Kuna watu mpaka leo wanasema eti Yanga ina pengo la Fiston Mayele na inatakiwa itafute straika kama yeye, hii si kweli kwa sababu Nabi alikuwa na mfumo wake ambao ulitegemea kumzunguka yeye, tofauti na [Miguel] Gamondi ambaye amekuja kuibadilisha kwa kuvuna mabao kutoka maeneo mbalimbali, mawinga, viungo washambuliaji na mabeki wote wanafunga mabao.

"Nimeona wengi wanauliza kama tumekata kiu ya Fiston Mayele, kwanza tujiulize kazi ya Mayele nchini ilikuwa nini? Lakini hivi tunavyozungumza kwenye msimamo wa orodha ya wafungaji mabao, kinara anatoka kwenye Klabu ya Yanga, ambaye ni Stephane Aziz Ki, akifunga jumla ya mabao 10 mpaka sasa.

"Kitu ambacho Gamondi amejitofautisha na Nabi ni kwamba mabao hayatoki sehemu moja, sasa hivi mabao yanatoka sehemu tofauti za uwanja, sasa hivi Maxi Nzengeli, Pacome Zouzoua, Aziz Ki na ndiyo maana utaona msimu huu namba ya mabao ni kubwa kwa sababu mabao yanatoka sehemu nyingi," alisema Kamwe.

Alisema wengi wanaodai bado kuna pengo la Mayele ni wale waliozoea kumuona mchezaji namba tisa amekaa mbele na kufunga mabao kitu ambacho kilikuwa kinafanywa na mchezaji huyo msimu uliopita, lakini anapokamatwa vizuri na mabeki timu inakosa matokeo mazuri.

"Watu wamezoea mtu avae namba tisa, akae pale mbele afunge, ndiyo maana baadhi ya mashabiki na wachambuzi wakawa wanasema Yanga haina mshambuliaji, lakini tunaongoza kwa mabao."

Alisema Guede wamemwongeza hasa kwa ajili ya mechi za kimataifa, kwa kuwa wanatakiwa nguvu iongezeke kwa sababu viungo washambuliaji wao wanaofunga mabao wanaweza kubanwa sana, na ukiwa na straika ambaye anatumia nafasi chache tu zinazopatikana wanaweza kutoka na ushindi.

Yanga imemsajili straika huyo dirisha dogo la usajili kuchukua nafasi ya straika Mghana Hafiz Konkoni, ambaye naye alisajiliwa baada ya klabu hiyo kumuuza Mayele kuelekea Pyramids ya Misri.

## Benchikha kuishushia Tembo straika wapya

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikishuka Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam leo majira ya saa moja usiku dhidi ya Tembo FC ya Tabora, kwenye mechi ya hatua ya 32 ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), maarufu FA Cup, Kocha Mkuu wa miamba hiyo, Abdelhak Benchikha, anatarajia kuanzisha 'majembe' yake mapya.

Simba itashuka dimbani kwa mara ya kwanza tangu Januari 13, mwaka huu ilipocheza mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar na kufungwa bao 1-0 dhidi ya Mlandege, lakini itakuwa ni mara ya kwanza kwa mashabiki wa Dar es Salaam kuiona timu hiyo tangu ilipocheza mechi yake ya Ligi Kuu, Desemba 23, mwaka jana,

INAENDELEA UK. 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042